# Nipashe

Jumanne Novemba 19, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581865

The Guardian digital

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com




UKURASA WA 4

**Wauzaji** maji Dar walalama bidhaa yao kuadimika




UKURASA WA 3

**Wawasilisha** hoja mahakamani kesi kigogo wa JATU ifutwe kisheria



UKURASA WA 8

**EU** yatoa bilioni 6.9/- upatikanaji nishati safi ya kupikia Tanzania

JENGO LILILOPOROMOKA...

# Hali tete wapigaji michango maafa



- **Waziri** Mkuu aagiza Niffer akamatwe, miili ya watu 15 kati ya 16 yaagwa; Chalamila asema yuko tayari kuwajibika ikiwa... *Ukurasa 2*



Mejeneza yenye miili ya walioangukiwa na jengo la biashara Kariakoo jijini Da es Salaam yakiwa yamepangwa kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kuagwa jana. **PICHA: PICHA: JUMANNE JUMA**

# TANESCO yataja sababu umeme kukatika mara kwa mara

UKURASA 4





Skani hapa kutembelea chaneli yetu


# Silaa aahidi ushirikiano na vyombo vya habari

UK. 3

**MICHEZO** **TAIFA STARS KUFA KUPONA LEO** UK.24

**MAONI,** UK.6



Baadhi ya waombolezaji wakilia wakati wa kuaga miili ya watu waliokufa kwenye ajali ya kuanguka kwa jengo la ghorofa eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

JENGO LILILOPOROMOKA...

# Hali tete wapigaji michango ya maafa

**Na Halfani Chusi**

WATU wanaogeuza majanga ya kitaifa kuwa fursa ya kujipatia kipato, wamekumbana na mkono wa dola:

Waziri Mkuu amewataka watanzania kuacha kuchangisha wananchi kupata fedha za kusaidia uokoaji katika jengo lililoporomoka Kariakoo, jijini Dar es Salaam.

Amesema serikali ina utaratibu wa utoaji misaada kupitia Kamati ya Maafa iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na akaunti hiyo iko Benki Kuu ya Tanzania (BoT), hivyo akaeleza kukamatwa mara moja kwa waliobainika kuchangisha michango hiyo.

"Yuko binti anaitwa Niffer (Jenifer Jovin) atafutwe aeleze nani alimpa kibali cha kuchangisha umma, amekusanya shilingi ngapi, amezipeleka wapi na kwanini amefanya hivyo," Majaliwa aliagiza.

Waziri Mkuu alitoa kauli hiyo baada ya kukagua mwendelezo wa uokoaji katika jengo hilo lililoporomoka Novemba 16 mwaka huu na baadaye kuongoza kuaga miili ya watu 15 kati ya 16 waliofariki dunia kutokana na tukio hilo, akisisitiza zoezi hilo ni endelevu hadi atakapookolewa mtu wa mwisho.

"Tumeanza kuwaona watu wachache wanatumia majanga haya kama fursa. Ninaliagiza Jeshi la Polisi limtafute aseme amekusanya shilingi ngapi? Amepata kibali wapi na fedha amezifanyia nini" Majaliwa alitamka kwa ukali huku Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo akionesha ishara ya kupokea maagizo.

Waziri Mkuu aliwashukuru watu binafsi, mashirika ya umma, vyombo vya uokoaji, ulinzi na usalama kwa kujitolea katika kufanya uokoaji mara tu baada ya tukio kutokea.

Aliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha linamtafuta mmiliki wa jengo hilo ili asaidie timu ya uchunguzi kufahamu kuhusu chanzo cha kuporomoka kwa jengo hilo.

Pia alisema kuwa hadi jana asubuhi, jumla ya watu 86 walikuwa wameokolewa. Kati yao, watano wanaendelea na matibabu, pamoja na hao 16 wamefariki dunia.

**TIMU YA UCHUNGUZI**

Waziri Mkuu alisema wakati zoezi la uokoaji likiendelea, tayari serikali imeunda timu ya watu 19 ya uchunguzi ikiwa ni utekelezaji agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kufanya uchunguzi kujua chanzo cha kudondoka kwa jengo hilo.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, timu hiyo ya uchunguzi inaongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Brigedia Generali Hosea Ndagala.

"Timu hii pia itakagua uimara wa majengo yote yaliyojengwa na yanayoendelea kujengwa katika eneo lote la Kariakoo, Waziri Mkuu alisema bila kutaja muda ambao timu hiyo imepewa kufanya uchunguzi.

Alisema timu iliyoundwa itazunguka eneo lote la Kariakoo na kufanya ukaguzi wa majengo na baadaye kutoa ushauri wa nini cha kufanya ili yasitokee majanga mengine kama hayo.

Majaliwa alisema Kariakoo ni soko la kimataifa, hivyo serikali haina budi kulilinda na wafanyabiashara wake.

Baada ya kukagua maendeleo ya uokoaji katika eneo la Kariakoo, Majaliwa aliwaongoza wananchi kuaga miili 15 kati ya 16 waliofariki dunia kutokana na kuporomoka kwa jengo hadi kufikia jana saa tatu asubuhi.

Alisema serikali inagharamia matibabu kwa majeruhi wote pamoja na huduma ya mazishi kwa miili ya marehemu wote wa ajali hiyo.

Awali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi, alisema serikali inaendelea kuratibu shughuli za uokoaji ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za haraka ili kusaidia zoezi hilo.

Alisema kuwa serikali kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama imeendelea kuratibu mazoezi ya utafutaji na uokoaji, kutoa huduma ya kwanza na kuwafikisha hospitalini, kutoa huduma za kijamii pamoja na kuwezesha mitungi ya gesi ya oksijeni kwa ajili ya watu walioko chini ya kifusi.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Kariakoo, Martine Mbwana, alimshukuru Rais Samia na serikali kwa ujumla kwa hatua alizozichukua na msaada waliotoa tangu kutokea kwa ajali hiyo.

**RC CHALAMILA**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema yuko tayari kuwajibika iwapo uchunguzi utabaini yeye na timu yake hawakufanya kazi ipasavyo katika uokoaji.

Akizungumza wakati wa kuaga miili hiyo, Chalamila alisema anafikiri yeye na timu yake wamefanya kazi ya uokoaji hadi walipofikia.

Hivyo, akasisitiza kwamba kama uchunguzi utabaini hawakufanya kazi ipasavyo yuko tayari kuwajibika.

"Mpaka sasa tunaendelea na uokoaji, baada ya jengo kuanguka ilitulazimu tuamuru lisibomolewe ili tutumie akili ya uokoaji.

"Kuna watu wengi waliona hatuwajibiki ipasavyo, niombe pale ambao utabaini hatukuwajibika nitakuwa tayari kuwajibika," alisema Chalamila mbele ya Waziri Mkuu Majaliwa.

Alisema hadi jana saa sita mchana, alikuwa na dereva wa Uber aliyewapigia simu akiwa ndani ya jengo hilo kabla ya kuokolewa.

"Akiwa ndani ya jengo, alituambia nguvu inaniishia, yeye na watu wengine na hivi ninavyozungumza tumewaokoa na wote wako hospitalini.

"Watu wanahisi waliopoteza maisha walichelewa kuokolewa na kina Chalamila, ndio maana wamefariki (dunia). Madaktari ni mashahidi, wengi waliofariki dunia baada ya tukio, waliangukiwa na matofali ya kutoka ghorofani ambao majeraha hayo yalisababisha vifo vyao.

"Sisi ni wanadamu, yawezekana kuna watu nimewakwaza, ninaomba nirudie tena, nipo tayari kuwajibika," alisema Chalamila kwa hisia kali.

Mkuu wa Mkoa huyo aliwatoa hofu wafanyabiashara na watu wote waliofikwa na majanga kwamba hakuna mzigo utakaopotea.

**VILIO, SIMANZI**

Wakati wa kuaga miili ya watu 15 kati ya 16, vilio na simanzi vilitawala miongoni mwa mamia ya watanzania waliofurika kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini.

Nyuso za waombolezaji zilionesha simanzi, Mkuu wa Mkoa Chalamila akitumia nafasi hiyo kuwafariji na kuwaambia jitihada za kuwaokoa ambao wako chini ya ardhi zinaendelea.

Katika eneo hilo, ndugu walikuwa wanajitokeza na kukabidhiwa miili kwa ajili ya safari ya kwenda kuwapumzisha ndugu zao.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Wawasilisha hoja mahakamani kesi ya kigogo wa JATU ifutwe

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeutaka upande wa mashtaka kuharakisha upelelezi wa kesi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya JATU Public Limited, Peter Gasaya.

Hakimu Mkazi Mwandamizi Godfrey Mhini aliyasema hayo jana wakati kesi hiyo ilipotajwa, kisha upande wa mashtaka ukiwakilishwa na Wakili wa Serikali Roida Mwakamele ukadai haujakamilisha upelelezi.

Baada ya kudai hayo, Wakili wa Utetezi Nafikile Mwamboma alidai kuwa, mara ya mwisho upande wa jamhuri ulitakiwa kuja kueleza hatua ya upelelezi ulipofikia na si kueleza upelelezi haujakamilika.

Wakili huyo alidai kesi hiyo ilishafutwa na kufunguliwa upya, hivyo ilipaswa kuanza kusikilizwa na si kuwa hatua ya upelelezi.

"Mahakama hii ina wajibu wa kusimamia mwenendo wake wa kesi, kusema jalada halijawafikia si sawa, tunaomba mahakama ifute shtaka na imwachie mshtakiwa," alidai Wakili Mwamboma.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Roida alidai jalada la kesi hiyo halijawafikia; ndio maana hawajui hatua ilipofikia.

Ndipo hakimu aliutaka upande wa jamhuri kuharakisha upelelezi. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Desemba 2, mwaka huu.

Katika kesi hiyo, Gasaya anadaiwa kuwa kati ya Januari Mosi, 2020 hadi Desemba 31, 2021, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa kama Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, alijipatia Sh. 5,139,865,733 kutoka Saccos ya JATU kwa njia ya udanganyifu.

Ilidaiwa kwamba, alijipatia kiasi hicho cha fedha kwa madai kwamba atakizalisha kwa kuwekeza katika mazao ya kilimo na kupata faida zaidi, jambo ambalo alijua si kweli.

Katika shitaka la pili, ilidaiwa kwamba, Gasaya alitakatisha fedha hizo zilizokuwa katika akaunti ya JATU iliyoko benki ya NMB tawi la Temeke, kwa kujihusisha katika miamala.

Ilidaiwa kuwa alifanya hivyo huku akijua fedha hizo ni mazalia ya kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Mwongozo wa Utendaji wa Mahakama unaelekeza kesi za kawaida zisikilizwe na kutolewa uamuzi ndani ya miezi sita tangu kufunguliwa kwake na kesi kubwa zisikilizwe kwa muda usiozidi mwaka mmoja.



*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/ sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Silaa aahidi ushirikiano na vyombo vya habari

**Na Maulid Mmbaga**

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeahidi ushirikiano na wadau mbalimbali wa sekta hiyo ikiwamo vyombo na wanahabari, ili kuhakikisha mazingira rafiki wakati wa utekelezaji wa majukumu kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Jerry Silaa, wakati wa mkutano wa wadau wa sekta ya habari, alisema anatarajia Novemba 21, mwaka huu, kukutana na Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa, ambao ndani kuna taasisi 16 kujadili masuala mbalimbali ya kisekta.

Alisema baadaye atakutana pia na taasisi moja kati ya 1,023 za nchini, akieleza kuwa sekta ya habari ni mtambuka na inasimamiwa na sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ambazo katika utekelezaji wake wanahabari wanafurahia haki na uhuru wa kupata na kupasha habari bila kuwa na woga wa kijinai.

"Kutokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, Septemba 14, mwaka huu, nimeteua pia wajumbe sita wa bodi itakayosaidia masuala mbalimbali katika sekta hii, na hii itatufungulia safari ya kuanzisha meza huru na mfuko wa tathmini ya uchumi kwa wanahabari.

"Pia wizara inaendelea kuratibu uendeshaji wa mchakato wa maboresho ya sera ya habari, haya ni kati ya masuala ya msingi yanayokwenda kuboresha sekta ya habari nchini, ili kukamilisha jukumu la wanahabari kuhakikisha wananchi wanapata habari sahihi na kwa wakati, na kuwa huru kwa mujibu wa sheria," alisema Silaa.

Aliongeza kuwa Tanzania imekuwa mfano wa kuigwa katika suala la amani na kuimarisha mshikamano na umoja wa kitaifa kwa mchango wa vyombo vya habari.

"Niwaahidi sisi ni familia moja, niko karibu nanyi, milango yangu iko wazi karibuni tujenge sekta yetu," alisisitiza Silaa.

Aidha, alisema ni dhamira yake kuhakikisha wanafanya mapinduzi katika sekta ya habari, na kwamba wameanza na sera na sheria, pamoja na kuendelea kuvisikiliza vyombo mbalimbali kukaa kuzungumza na kubadilishana uzoefu ili kuifanya sekta hiyo kuwa bora zaidi.

Rais wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzani (UTPC), Kenneth Simbeye, alitoa mapendekezo ya umoja huo kuelekea uchaguzi wa Serikali ya Mitaa na Uchaguzi Mkuu, kwamba vyombo vya habari viwezeshwe kutekeleza wajibu wao kwa weledi bila kubugudhiwa, na waandishi kuachwa watimize majukumu yao kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya kitaaluma.



Alishauri chombo cha habari kisibaguliwe kwa mtazamo wa kidini au siasa, waandishi waheshimiwe, pamoja na wasimamizi wa vyombo hivyo wasimamie kwa usawa bila kujali kwamba ni cha serikali au binafsi.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alisema kuelekea uchaguzi watahakikisha wanatimiza wajibu wao wa kusimamia sheria na kutengeneza mazingira ya amani na kuzuia viashiria vya uhalifu kabla havijatokea.

Alisema lengo la Jeshi la Polisi sio kutekeleza majukumu hayo kwenye uchaguzi pekee bali hata baada ya uchaguzi na kwamba watahakikisha usalama wa wagombea wakati wa kampeni, wapiga kura na hata katika hatua ya kuhesabu kura.

"Wajibu wetu pia ni kuweka ushirikiano mzuri na vyombo vya habari wakiwamo waandishi wa habari. Pia tutawaandaa askari kwa nadharia na vitendo lengo ni kuwezesha uchaguzi kufanyika kwa amani na usalama," aliahidi Misime.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imepokea maombi ya leseni ya muda ya kuzalisha umeme kutoka kwa Kampuni iliyotajwa hapo chini. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kuhusiana na maombi hayo ya leseni. Taarifa za mwombaji pamoja na aina ya leseni iliyoombwa ni kama inavyoonekana hapa chini:

| Na. | MAELEZO |
|---|---|
| Jina na anuani ya Mwombaji | ARMSTONE HYDRO LIMITED,<br>S.L.P 75396, KINONDONI – DAR ES SALAAM. |
| Eneo | Kijiji cha Njomulole/Kanyoni, Kata ya Muhange, Wilaya ya Kakonko katika Mkoa wa Kigoma |
| Taarifa za Wanahisa | 1) ARMSTONE HOLDINGS COMPANY,<br>S.L.P 75396, DAR ES SALAAM, Hisa **98%**<br>2) JOSEPH NYONYI LUJARA,<br>S.L.P 75396, DAR ES SALAAM, Hisa **1%**<br>3) DK. GELARD JACOB<br>S.L.P 75396, DAR ES SALAAM, Hisa **1%** |
| Maelezo ya Mtambo na Matumizi | Kuzalisha umeme wa Megawati 3.0 kwa Nishati ya Maji.<br>Umeme utakaozalishwa utauzwa kwa TANESCO na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa kwa ajili ya usambazaji |
| Aina na Muda wa Leseni | Leseni ya muda mfupi ya kufanya maandalizi ya kuzalisha umeme kwa miaka mitatu (3) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi haya awasilishe kwa maandishi kwa anuani iliyopo hapa chini, ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Maombi ya leseni yanaweza kuoneshwa kwa mtu kwa maombi maalum ya maandishi.

**Jengo la EWURA, 3 Barabara ya EWURA, 41104 Tambukareli, S.L.P 2857, Dodoma, Tanzania**
**Simu: +255 26 2329002 - 4, Nukushi: +255 26 2329005**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**

# Wauzaji maji Dar walia 'bidhaa yao' kuadimika

**Na Beatrice Moses**

BAADHI ya wafanyabiashara wanaouza maji wanayohifadhi katika matangi ya kubebwa na magari maarufu maboza, mkoani Dar es Salaam, wamelalama hali ni mbaya kibiashara kutokana na maji kuadimika.

Katika mazungumzo na Nipashe, wafanyabiashara hao wamedai kuwa kuadimika kwa bidhaa yao hiyo kunawapa wakati mgumu kwa kuwa ndio tegemeo lao kujipatia kipato cha kuendesha familia.

"Juzi, kutwa nzima maji hayakuwapo. Hapa si unaona hata ukingaji ulivyo, sivyo ambavyo huwa yanakingwa kwenye gari, huo mpira ulipaswa kuingizwa kwa juu kule, yana presha ndogo, hapa sina uhakika kama boza langu litajaa," alilalama Ezron Mmari, aliyejitambulisha amefanya biashara hiyo kwa miaka 20 sasa.

Akiwa kioski cha kujaza maji cha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kilichoko Mbezi TANESCO, Mmari alisema kuwa kipindi hiki ni kigumu kwao, hata wanalazimika kwenda kutafuta maji mbali, ikiwamo Kibamba, hivyo gharama zinakuwa kubwa tofauti miaka iliyopita.

Mmari alisema kuwa awali alikuwa anafanya kazi usiku na mchana na alikuwa anauza maboza 10 kwa siku, lakini sasa anauza maboza mawili hadi matatu kwa siku.

"Hatuna mazoea ya kuuza kwenye ndoo, inachukua muda mwingi, haina faida kwetu kwa kuwa inamzunguko mrefu na gharama. Mahitaji ni mengi, lakini kuyapata maji kwa sasa ni shida, hakuna uhakika," alisema.

Alifafanua kuwa boza la gari lake lina ujazo wa lita 10,000 ambazo huuza kwa bei ya kati ya Sh. Sh. 80,000 na Sh. 130,000 kulingana na umbali aliko mteja husika.

Dereva Amani Mdulu alisema wateja wapo katika maeneo tofauti, yakiwamo ambayo tayari yana mabomba lakini hayatoi maji. Pia maeneo ambayo hawajafungiwa mabomba ya maji na mamlaka.

Aliyataka maeneo yenye uhitaji mkubwa wa huduma hiyo kuwa ni pamoja na Msumi kwa Chinga, Pombo au Pangaboi.

"Kutoka hapa (Mbezi TANESCO) hadi kule (kuliko na uhitaji wa maji) ni umbali wa kama Km 20, unaweza kutia mafuta ya Sh. 30,000. Hapo sasa huwezi kuuza kwa bei waliyopanga serikali ya Sh. 15,000 kwa dumu la lita 1,000.

"Utauza hadi kwa Sh. 20,000 kwa dumu, hivyo kwa kuwa gari linabeba madumu matatu, unapata Sh. 60,000. Unakuwa na fedha inabaki ukitoa gharama za mafuta," alisema.

Madulu alisema kuwa katika vioski vya maji, wanauziwa lita 1,000 kwa Sh. 2,000. Alisema serikali wakati inapanga bei hiyo, kulikuwa na vioksi vingi vya maji, lakini hivi sasa vipo baadhi vimefungwa, akivitaja vya Wazo na Mbezi; kwamba sasa vimevunjwa kutokana na ujenzi wa barabara.

Madulu alisema kuwa kuna wakati kutokana na uhaba wa maji, hulazimika kuuza maji kwa anayetoa fedha nyingi.

"Huwa inatokea unapeleka maji mahali unakutana na mtu mwingine naye anahitaji, anakuuliza 'huyo atakupa shilingi ngapi? Basi mimi nitakupa Sh. 70,000 au 80,000 kwa madumu yote matatu', tunakatisha safari tunauza hapohapo," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano DAWASA, Everlasting Lyaro, alisema kuwa sababu ya kukatika kwa maji ni maboresho ya dharura yaliyokuwa yanafanywa katika mitambo yao ya kuzalishia huduma hiyo.

"Inapotokea dharura hulazimu kufanya maboresho, na maboresho haya yamefanyika zaidi katika Mtambo wa Ruvu Juu ambao uko Mlandizi, mkoani Pwani," alisema.

Everlasting alisema mfumo wa miundombinu ya maji katika vioski hupata maji moja kwa moja kutoka katika bomba kubwa, wakati watumiaji wa kawaida hupata maji kutoka katika mabomba madogo yaliyounganishwa kutoka bomba kubwa.

Alitaja vioski vya kutekea maji Dar es Salaam na Pwani viko Mbezi Beach Makonde, Tegeta Kibaoni, Salasala, Kihampa 1 (Kibamba), Terminal (Makongo), Kimara Suka, Kimara Spencon, Mpiji (Mapinga), Mlandizi, Kibaha na Chalinze. Gharama ya uniti moja ya maji (lita 1,000) ni Sh. 1,106.



Baadhi ya wafanyabiashara wa maji wakijaza maji kwenye magari yao katika kioski cha Mbezi Beach, Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE MOSES**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# THRDC yaridhishwa changamoto Ngorongoro kushughulikiwa

**Na Mwandishi Wetu**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umesema umebaini changamoto za kuwahudumia wananchi Tarafa ya Ngorongoro, zimeanza kushughulikiwa hasa huduma za msingi.

Umesema pamoja na ukarabati wa maeneo mengi ya huduma za kijamii haujaanza, umejionea mikakati na hatua za awali za urejeshwaji wa huduma za msingi.

"Hali ya huduma za kijamii miezi miwili baada ya agizo la Rais, tunapenda kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa hatua nzuri aliyoichukua ya kutuma wajumbe wake wakati wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro, wakiwa katika maandamano yaliyodumu kwa siku tano.

"Uamuzi huo wa kutuma watu wa kusikiliza vilio vya wananchi na kuagiza vilio vyao vifanyiwe kazi vimeonyesha busara na hekima ya Rais. Kwa muda mrefu watetezi wa haki za binadamu tumekuwa tukishauri uongozi wa juu wa nchi ukutane na wananchi, baada ya Rais kutuma wajumbe wake tumeanza kuona faida ya hatua hii kwa wananchi wa tarafa hii.

Pamoja na kwamba serikali ndio imelalamikiwa kusababisha changamoto hizi, kitendo cha Rais kuamua vikwazo hivi viondelewe imeleta matumaini mapya kwa watu wa Ngorongoro, kimetufurahisha sisi watetezi wa haki za binadamu na pia hatua hii inalinda taswira ya nchi katika eneo la haki za binadamu na utawala bora," ulisema mtandao huo.

Aidha, baada ya kufanya ziara mwaka 2024 katika Tarafa ya Ngorongoro, THRDC umejionea hali ya haki za binadamu pamoja na huduma za kijamii katika tarafa ya Ngorongoro.

"Tunatambua na kuthamini juhudi za hivi karibuni zilizofanywa na serikali kurejesha huduma muhimu za kijamii katika Tarafa ya Ngorongoro, eneo ambalo liliathiriwa kwa kiasi kikubwa na kusitishwa kwa huduma hizi kwa takriban mwaka mzima.

"Kusitishwa kwa huduma hizo hasa kuanzia mwaka 2022 kuliathiri jamii za asili na wafugaji katika eneo hilo ambalo ni mseto. Tarafa ya Ngorongoro yenye idadi ya watu 100,000 ina jumla ya kata 11, vijiji 25, shule za msingi 22, shule za sekondari tatu, hospitali moja ya Misheni na vituo vya afya na zahanati 13.

"Vyote hivi vimekuwa na changamoto nyingi za kuwahudumia wananchi kwa miaka minne sasa. Pamoja na kwamba bado ukarabati wa maeneo mengi ya huduma za kijamii haujaanza."

# Tanesco yataja sababu umeme kukatika mara kwa mara

**Na Grace Gurisha**

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, amesema matumizi ya umeme yameongezeka kutoka asilimia sita hadi 16 kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Aidha, amesema hali hiyo ndio imesababisha serikali kuwa na miradi katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kuboresha njia za upatikanaji wa umeme ili kuondoa tatizo hususani katika eneo la Mbagala, Gongolamboto, Dege Kigamboni na Mkuranga.

Alisema hayo jana alipotembelea kituo cha umeme wa gesi asilia wa Kinyerezi Moja kuangalia matengenezo yaliyokuwa yakiendelea ya kufunga transfoma mbili za ukubwa wa MVA 350, moja ina MVA 175.

"Kuna baadhi ya maeneo kumekuwa na hali ya umeme ya kutoridhisha na hiyo yote ni kwa ajili ya kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi, uzalishaji na kijamii.

"Matumizi ya umeme yamekuwa yakipanda kwa kasi kubwa sana ndio maana imetulazimu kila baada ya muda kuwa na miradi ambayo itaboresha upatikanaji wa umeme mkoani hapa," alisema Kapinga.

Alisema hakuna tatizo la umeme, upo lakini ililazimika kufunga njia za kwa ajili ya kuboresha huduma hiyo ili waweze kufunga transfoma hizo.

"Tumefika hapa kwa ajili ya kuona mradi huu unaendelea na nyie wote mnafahamu hapo nyuma mwaka 2015 tulikuwa na mradi wa kuongeza uwezo wa kituo hiki cha umeme kwa kuweka Kinyerezi One ambayo inazalisha takribani megawati 185 na leo uwezo wa kituo umepanda kufikia megawatinl 375," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Gissima Nyamo-Hanga, alisema wanazalisha umeme mwingi unaopelekwa Ubungo kwa ajili ya kugawa kwenye maeneo hayo, lakini sehemu yake unaotokea Kinyerezi kwenda Mbagala kupitia Gongolamboto.

"Lakini ukiondokea hapa kupitia Gongolamboto unaweza kwenda mpaka Mkuranga ukaenda pia hadi Kigamboni.

Ukuaji wa umeme umekuwa ni mkubwa sana hasa kuanzishwa kwa viwanda vingi katika maeneo ya Mkuranga.

" Tulichokuwa tunakifanya hapa baada ya kuona matumizi ya umeme maeneo hayo yanakuwa makubwa sana serikali yetu tukawa tumeleta transfoma nyingine kubwa mbili katika kituo hiki kulikuwa na transfoma ya MVA 50 kutokana na kuzidiwa huko kulitokana na kukua kwa mahitaji tumeleta transfoma mbili kila moja ina ukubwa wa 175," alisema.

## Ujambazi wampeleka jela miaka 30

**Na Daniel Limbe,**
BIHARAMULO

MAKAHAMA ya Wilaya ya Biharamulo, mkoani Kagera imemhukumu kifungo cha miaka 30 gerezani Mashaka Samwel (20), mkazi wa kijiji cha Nyakasenga, wilayani Geita baada ya kukutwa na hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Subira Mashambo baada ya kujiridhisha pasi na shaka na ushahidi uliowasilishwa na upande wa mashtaka.

Awali Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mashitaka Wilaya ya Biharamulo, Wakili Edith Tuka, akishirikiana na Suddy Lugano, walidai mahakamani kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Agosti Mosi 2023 katika kijiji cha Nyabugombe, wilayani Biharamulom, akipora Sh. milioni 1.5.

"Mnamo Agosti Mosi, 2023, saa tano usiku huko katika kijiji cha Nyabugombe, mshtakiwa Mashaka Samwel, alifika nyumbani kwa mwathiriwa wa tukio (jina tunalihifadhi) akiwa na silaha ya moto, alimvamia na kumshikilia kwa zaidi ya saa sita, akimtaka kutoa fedha zote alizokuwa nazo," alidai.

Editi alidai kuwa katika kunusuru maisha yake, mwathiriwa alilazimika kutoa Sh. milioni 1.5 na ndipo alipoachiwa huru na mshtakiwa kuondoka eneo la tukio kabla ya kukamatwa na kitengo maalumu cha upelelezi kwa njia ya mtandao cha Jeshi la Polisi wakati akiendelea kutuma fedha kwenye namba za simu ambazo tunazihifadhi.

Baada ya mshtakiwa kufikishwa mahakamani, alisomewa mashtaka ya unyang'anyi wa kutumia silaha, jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa kifungu namba 287(a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Baada ya mahakama hiyo kujiridhisha na vielelezo vilivyowasilishwa, ilimpa nafasi mshtakiwa kujitetea ili apunguziwe adhabu ambako alidai ana familia na watoto wadogo wanaomtegemea na kwamba mahakama hiyo ione namna inavyoweza kumsaidia.

Pamoja na utetezi wake, Hakimu Subira Mashambo alimhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani ili liwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia kama hiyo.

# Vitanda, vibebeo vya watoto njiti changamoto hospitalini

**Na Maulid Mmbaga**

MUUGUZI katika wodi ya watoto njiti Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke, Benardetha Shine, amesema uhaba wa eneo, vitanda na vibebeo vya kangaroo ni miongoni mwa changamoto zinazowakabili na kushindwa kupokea idadi kubwa ya wagonjwa wa aina hiyo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika uzinduzi wa programu ya usambazaji wa mifuko ya kangaroo inayotumika kubebea watoto waliozaliwa kabla ya muda, inayoratibiwa na Taasisi ya Babymoon, muuguzi huyo alisema wakipata vibebeo kwa wingi itasaidia kukabiliana na tatizo hilo kwa kuwa wazazi wataruhusiwa kwa wakati.

Alisema wazazi wengi wanaporuhusiwa wanaomba wapatiwe vibebeo hivyo, lakini kutokana na uhaba uliopo wanashindwa, akieleza kuwa ni matumaini yake vikipatikana vya kutosha itasaidia wazazi kutumia muda mfupi, kuruhusiwa kwa wakati pamoja na kutoa nafasi kwa wengine kupata huduma.

"Kwa miaka 12 sasa nimekaa wodi ya watoto wa aina hiyo, anaweza kuongezeka gramu 30 hadi 50 kwa siku anapobebwa na vibebeo hivyo, mama anaweza kukaa na kangaroo kwa wiki mbili halafu akaruhusiwa, hivyo ili kurahisisha ubebaji wa watoto hawa tunahitaji sana bidhaa hiyo.

"Tunaomba wadau mbalimbali pamoja na viongozi wa serikali na taasisi binafsi tusaidiane kwa ajili ya kupata hivi vibebeo kwa manufaa ya watoto hawa ambao ni kizazi cha kesho, mimi mwenyewe nitaenda kutafuta chochote kitu ili niwasaidie, tusipowekeza kwa watoto wachanga tujue taifa la kesho hatuna," alisema Benardetha.

Aidha, wanatamani wazazi hao wangeruhusiwa kwenda nyumbani na vibebeo hivyo kwa sababu haiwezekani kukaa hospitalini mpaka apate kilo 2.5, badala yake wanamwelimisha mama, baba, na ndugu wengine namna ya kubeba mtoto ili atakapofikia kilo 1.5 aruhusuwe apishe wengine.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Dk. Debora Maufi, alisema programu hiyo inalenga kuboresha afya ya watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya wakati au wakiwa na uzito pungufu, na kwamba njia ya Kangaroo ni ya kiasili ambayo imekuwa na matokeo chanya katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kwa Tanzania tunaona kuna changamoto kubwa kuna watoto zaidi ya 370,000 wanazaliwa kila mwaka wakiwa na tatizo hilo, na nadhani ni muhimu sana endapo tutaungana kwa ajili ya kutatua changamoto hiyo, tunatarajia kufikia familia 20,000 kwa hatua ya awali," alisema Dk. Debora.

Miongoni mwa wazazi waliojifungua mtoto kabla ya wakati, Witness Kilonzo, alisema alijifungua mwanawe akiwa na miezi sita ya ujauzito, na huduma ya Kangaroo ilimsaidia kumkuza kwa haraka kwa kuwa zina tabaka mbili maalumu inayohifadhi joto lisipotee.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jim Yonazi, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuhusu hali ya uokoaji inavyoendelea katika ghorofa lililoporomoka eneo la Kariakoo na kuwataka watu wanaochangisha fedha kwa ajili ya janga hilo wafuate utaratibu wa kisheria na 'account' ya kukusanyia fedha iwe moja tu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# ...Taasisi yazindua mtandao familia watoto njiti

**Na Frank Monyo**

KATIKA kilele cha Siku ya Mtoto Njiti, kilichohitimishwa jana, Taasisi ya Doris Mollel Foundation imezindua Mtandao wa Familia za Watoto Njiti nchini ili kutoa elimu, msaada na kuhamasisha jamii kuhusu changamoto zinazowakumba watoto njiti ili kukuza uelewa.

Mtandao huo utawaleta wazazi na familia za watoto njiti kushirikiana, kubadilishana uzoefu na kupewa msaada wa kitaalamu katika huduma za afya, hasa katika muktadha wa huduma bora kwa watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.

Akizindua mtandao huo jana jijini Dar es Salaam, tukio lililotanguliwa na mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu kuandika habari za watoto njiti, Daktari Bingwa wa Watoto na Mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Doris Mollel Foundation, Albert Chota, alisema lengo lingine la mtandao huo ni kuisaidia serikali kupunguza vifo na kuielemisha jamii kuhusu watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti).

Alisema ni wajibu wa serikali kuongeza idadi ya wahudumu wa afya, ambao wataisaidia kuokoa maisha ya watoto njiti, akitoa mfano kuwa na uwiano wa 'mtoto njiti mmoja, muuguzi mmoja.'

"Kwa kupitia mtandao huu, familia zitapata taarifa muhimu kuhusu jinsi ya kushughulikia afya na ustawi wa watoto wao njiti, ikiwamo huduma za mapema na uangalizi wa afya kwa watoto hao. Doris Mollel, ambaye alikuwa mtoto njiti, alisisitiza umuhimu wa jamii kuwa na uelewa mkubwa kuhusu changamoto hizo na kuhamasisha serikali pamoja na wadau wa afya kutoa msaada wa kutosha," alisema.

Alisema mtandao huo pia utaongeza ufanisi wa kupunguza vifo vya watoto njiti kwa kutoa vifaa vya afya na msaada wa kiufundi kwa vituo vya afya na hospitali mbalimbali nchini.

"Juhudi hizi ni sehemu ya malengo ya Taasisi ya Doris Mollel Foundation ya kuboresha huduma za afya na kusaidia familia za watoto njiti kuwa na ufahamu na msaada unaohitajika.

Dk. Chota pia aliiomba serikali kuingilia kati suala la gharama za kuwahudumia watoto njiti hospitalini, gharama hizo zimekuwa kikwazo kwenye mapambano ya kupunguza vifo vitokanavyo na uangalizi finyu wa watoto hao.

Awali, mwakilishi kutoka taasisi hiyo, Dk. Sylvia Ruambo, akimwakilisha mwasisi wa taasisi hiyo, alisema katika mafanikio ya miaka tisa waliyoyapata tangu kuanzishwa kwake, tayari wamezifikia hospitali 85 nchi nzima katika kuchangia vifaa tiba kama mashine za kupumulia, vitanda n.k, vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.5.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi Serikali za Mitaa utoe taswira ya Uchaguzi Mkuu

**WAKATI** Watanzania wakitarajia kupiga kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Novemba 27, mwaka huu, ni vizuri uchaguzi huo ukatumika kuleta taswira nzuri kuelekea Uchaguzi Mkuu, mwaka 2025.

Uchaguzi huu utumike kujifunza dosari na mafanikio yaliyopatikana ili kama kulikuwa na changamoto zozote zisijitokeze katika Uchaguzi Mkuu.

Wakati wa mchakato wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kumekuwapo na dosari mbalimbali ambazo kama wananchi wangepata elimu ya kutosha zisingejitokeza.

Kulikuwa na malalamiko wakati wagombea wa vyama mbalimbali wakirudisha fomu kuenguliwa kwenye kinyang'anyiro kwa sababu ya kukosea kuzijaza.

Sisi tunaona kuwa tatizo kama hilo lingeweza kutatuliwa na maofisa waliokuwa wakipokea fomu hizo kwa kuwaelimisha wananchi kusahihisha fomu zao, badala ya kuwaengua labda kwa kukosea kuandika mwaka au tarehe yake ya kuzaliwa.

Mchakato wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, umetoa funzo pia kwa Tume Huru ya Uchaguzi (INEC), kuona kasoro hizo na kuanza kutoa elimu mapema ya umuhimu wa wananchi kusoma maelezo ya fomu wanazojaza kwa umakini na uelewa na kama hawajaelewa ni vizuri kuuliza ili waweze kueleweshwa.

Kama elimu itatolewa mapema na wananchi wakaelewa bila shaka kasoro hizo ndogo hazitajitokeza na malalamiko yanayotoka kwa wagombea wa vyama mbalimbali au mapingamizi hayawezi kuwapo.

Ni vizuri pia wananchi wakashiriki katika elimu zinazotolewa za umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi ili waweze kuelewa nini wanachotakiwa kufanya na nini hawatakiwi kukifanya.

INEC ina jukumu kubwa la kutoa elimu hii mapema ili wanaolalamika kutopata uelewa wasiwe na visingizio.

Pamoja na kutoa elimu kupitia vipeperushi, makala mbalimbali kwenye vyombo vya habari na vipindi vya radio na televisheni, bado kuna wananchi ambao hawana utamaduni wa kujifunza kupitia njia za kujisomea au kushiriki katika mijadala inayoendeshwa na serikali na taasisi zisizo za kiserikali kupata ufahamu wa masuala ya uchaguzi.

Jeshi la Polisi wananchi wanalitegemea sana kuhakikisha kuwa uchaguzi unakwenda vizuri kwa kupata usimamizi mzuri wa ulinzi na usalama.

Katika kufanikisha uchaguzi unakuwa huru na wa amani, wananchi pia wanatakiwa kuonesha ushirikiano na jeshi hilo kwa kutokuwa chanzo cha kusababisha jeshi hilo kutumia nguvu kuhakikisha amani inakuwapo.

Jambo la msingi la kuzingatia ni kufuata sheria na taratibu kuepusha aina yoyote itakayosababisha sintofahamu.

Inapotokea wananchi, vyama, jeshi la polisi kutoshirikiana na kutunishiana misuli, lazima kutatokea vurugu na atakayeathirika ni yule asiyefuata sheria.

Ni muhimu kujifunza kwa nchi za wenzetu ambazo zimefanya uchaguzi kwa amani na hata matokeo yalipotangazwa yalipokewa kwa amani na waliopinga walikwenda mahakamani badala ya kujichukulia sheria mkononi.

Mifano imeonekana kwa walioamua kuchukua sheria mkononi, vurugu zilizotokea na kusababisha baadhi kujeruhiwa na kupoteza maisha na vile vile nchi kuwa katika hali mbaya ya kiuchumi kutokana na mtikisiko uliosababishwa na vurugu hizo.

Serikali imeshatangaza kuwa dosari ndogo ndogo zilizojitokeza zirekebishwe ili uchaguzi wa Serikali za Mitaa ufanyike kwa amani na kila mgombea na mpigakura apate haki yake ya kimshingi ya kupiga kura na kuchaguliwa.

**Mungu ibariki Tanzania.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Shule, wazazi komesheni wanafunzi kuvaa kihuni

**WANAFUNZI** wanaosoma mijini ikiwamo Dar es Salaam, Mwanza na Arusha baadhi wanapunguza vipimo vya sare za shule ili viandane na jinsi wanavyotaka badala ya maelekezo ya shule.

Mtindo huo unawafanya wanafunzi wa kiume kubana suruali zao chini, huku wa kike wakipunguza sketi na kuzifupisha zikiwa juu ya magoti.

Hiyo ndio hatua ambayo baadhi ya wanafunzi wa sekondari wamefikia. Wazazi na walezi wanawashonea sare kulingana na maelekezo ya shule, lakini wanazifanyia mabadiliko kwa kuzibana au kupunguza urefu.

Lakini kwa kuwa baadhi ya shule ziko makini, huwachukulia hatua kwa kuzikata au kuzipasua kama njia ya kudhibiti vitendo hivyo, ambavyo ni utovu wa nidhamu.

Kwa kuwa mtindo huo wa kuharibu sare za shule unaendelea kufanywa na wanafunzi huku wengine wakining'iniza vitambaa kwenye mifuko ya nyuma, ni vyema wazazi na walezi wafuatilie mienendo ya watoto wao.

Ninaamini kwamba mzazi au mlezi anajua vipimo vya sare alizomshonea mtoto wake, kwa hiyo mtoto akivipunguza, ni rahisi kujua. Lakini inashangaza ni kwa nini mtindo huo unataka kuwa kama kwa kawaida?

**Kuvaa suruali mlegezo na kuning'iniza kitambaa mfuko, au kuvaa sketi fupi, ni mtindo uliozoeleka kufanywa na vijana wa kihuni, lakini ajabu ni kwamba baadhi ya wanafunzi nao wameanza kuiga.**

Imekuwa ni kawaida kuwakuta wanafunzi wakitoka nyumbani au shuleni wamevaa suruali mlegezo, huku chini ikiwa nyembamba kitambaa cha kufutia jasho kikining'inia kwenye mfuko wa nyuma wa suruali.

Je, wazazi na walezi hawajui vipimo vya suruali au sketi walizowashenea? Au hawafuatilii mienendo yao? Kwa nini wakubali watoto wao kwenda shuleni wakiwa wamevaa kihuni?

Kimsingi, nidhamu ni silaha katika masomo, kwani mwanafunzi mwenye nidhamu hufundishika na yule asiyetii hawezi kufundishika, kwa kuwa hawezi kusikiliza anachofundishwa na walimu wake.

Nidhamu shuleni ni kitu cha muhimu kwa maendeleo ya mwanafunzi, mwanafunzi asiye na nidhamu basi taaluma yake hushuka kumbukeni mwanafunzi hutengenezwa na mwalimu, wazazi, utawala wa shule na jamii.

Hivyo, suala la ushirikiano kwa makundi hayo ni wa muhimu ili kulinda nidhamu na maadili mema ya mwanafunzi, vinginevyo, nidhamu inaweza kuyumba na kusababisha kuporomoka kitaaluma.

Ikumbukwe kuwa moja ya njia ya kupitia ili kudhibiti utovu wa nidhamu kwa wanafunzi, ni kuangalia chanzo cha tatizo kabla ya kufikia kwenye uamuzi ambao mmojawapo ni adhabu.

Si vibaya wazazi na walezi wakaulizwa ili kujua kama wameshiriki kuwashonea watoto wao nguo ambazo zinakwenda kinyume na maelekezo ya shule, ili kama wanahusika, waambiwe ukweli.

Hicho ndicho nimeeleza kuwa ushirikiano wa wazazi, walezi na walimu ni jambo ambalo linapaswa kupewa kipaumbele, ikiwamo kuweka bayana kikanuni ili kulinda maadili mema.

Kuvaa suruali mlegezo na kuning'iniza kitambaa mfuko, au kuvaa sketi fupi, ni mtindo uliozoeleka kufanywa na vijana wa kihuni, lakini ajabu ni kwamba baadhi ya wanafunzi nao wameanza kuiga.

Sidhani kama ni busara kwa mwanafunzi kuvaa kwa mtindo huo unaosababisha hadi nguo zao ndani ziwe nje. Sasa kwa mwanafunzi kuwa wa aina hiyo, ni wazi hata katika masomo anaweza kujiharibia.

Mtu kuvaa suruali chini ya makalio, ina maana makalio yake unamwonesha nani? Ninadhani ni vyema wanafunzi wawachie wahuni mtindo huo, wao wajikite katika masomo tu.

Mwanafunzi kuvaa kwa heshima ni jambo la msingi kwa kuzingatia kwamba anaandaliwa kuwa mzazi bora na kiongozi mahiri wa miaka ijayo. Hivyo, ushirikiano ni muhimu kudhibiti wanafunzi kuvaa kihuni.

HABARI KITAIFA

## Wafanyabiashara walalama soko kutokuwa na uongozi wa kudumu

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

BAADHI ya wafanyabiashara wa soko la mnada wa mifugo na nyama choma Zinga, Halmashauri ya Bagamoyo, mkoani Pwani wamelalamikia kusuasua uchaguzi wa viongozi wa kudumu wa soko hilo.

Waziri Dihanga, mmoja wa wafanyabiashara hao waliozungumza na waandishi wa habari juzi kuhusiana na uhitaji wa viongozi wa soko, alisema viongozi watakuwa na mamlaka ya kuwawakilisha kufikisha mahitaji yao ngazi ya halmashauri.

Alidai kuwa mikutano mitatu imeshaitishwa kwa ajili ya kufanya mkutano wa uchaguzi, lakini inakwama kutokana na sababu mbalimbali ambazo ni kikwazo kufanikisha malengo yao.

"Kwenye hili soko lina miezi minne sasa tangu tugawiwe vizimba, kulikuwa na uongozi wa muda uliowekwa na halmashauri. Sasa tunataka kufanya uchaguzi, lakini kila ukipangwa, ushirikiano kutoka kwa viongozi waliopo unakosekana," alidai.

Ally Mustafa, mfanyabiashara katika soko hilo, alisema kuwa hivi sasa wanataka viongozi wa kudumu ili wafuatilie mustakabali wa vizimba katika soko hilo kwa kuwa walio wengi wanahitaji kuwa na vibanda vya kudumu.

Mustafa alidai uongozi wa muda unawarudisha nyuma kwa kutofanikisha uchaguzi kufanyika na hivyo wanashindwa kupata watetezi wa kufikisha malalamiko yao sehemu husika.

Mwenyekiti Msaidizi ambaye ni kati ya viongozi wa muda wa soko hilo, Abdulrazak Furahisha, alisema eneo hilo la serikali waliomba kwa ajili ya kufanyia mnada wa mifugo na nyama choma na kwamba baada ya kupatiwa, waliwagawia wafanyabiashara waliokuwa wanahitaji.

Furahisha alisema mkutano wa uchaguzi uliokuwa ufanyike Novemba 17, mwaka huu, ulikwama kwa mara nyingine baada ya kupigiwa simu na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Zinga ambaye alimwambia "hakuna uchaguzi na kwa sasa, viongozi waliopo waendelee".


Akizungumzia malalamiko hayo Ofisa Mtendaji wa Kata ya Zinga, Aziza Hemed alisema soko hilo linaendelea kuratibiwa na kila kinachofanyika ni kwa maelekezo ya Mkurugenzi na kwa sasa utaratibu unaoendelea ni kutangaza ili waendelee kuomba kupewa vizimba vya kufanyia biashara.

Alisema kwamba mwisho wa kupokea maombi ya wafanyabiashara kwa ajili ya kupata vizimba katika soko hilo ni Novemba 21, mwaka huu na baada ya hapo watapitia maombi na kuangalia vigezo kwa wataokidhi kupewa maeneo ya biashara.

Aziza, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alisema awali walifungua soko hilo kwa muda na kwamba Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inaandaa utaratibu wa kudumu wa kuendesha soko hilo.

"Huwezi kuundaa viongozi wakati utaratibu unaendelea, hadi hapo mkurugenzi atakapotoa utaratibu mwingine baada ya kukamilisha utaratibu wa kupokea maombi na kupitisha waliokidhi vigezo," alisema Aziza.

Alisema uongozi wa muda uliundwa kwa maelekezo ya mkurugenzi na kwamba taratibu zitakapokamilika, hatua za kupata viongozi wa kudumu zitafanyika kwa kuzingatia taratibu zilizoko.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji, akishiriki Mkutano wa Mashauriano wa Mawaziri wa Mazingira wa Afrika (AMCEN) juzi, uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa (COP29) unaoendelea jijini Baku, Azerbaijan. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Kanizio Manyika. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Familia yataka hatua wauaji mtendaji wa kijiji

**Na Halima Ikunji,** TABORA

JESHI la Polisi limesema limewakamata watu wawili wanaotuhumiwa kuhusika na mauaji ya aliyekuwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Nyahua Stesheni, wilayani Sikonge, Saidi Maduka, huku familia yake ikiomba serikali kuchukua hatua kali za kisheria.

Ofisa Mtendaji huyo alikutwa amefariki dunia huku mwili wake ukichomwa moto Septemba 9, mwaka huu, ikidaiwa kuwa mauaji yalifanywa wakati anapeleka wito kwa watuhumiwa kufika mahakamani kujibu mashtaka yanayowakabili.

Juzi wanafamilia, wakiongozwa na Juma Maduka, waliomba serikali kukamilisha uchunguzi na kutoa adhabu kali kwa waliofanya kitendo hicho.

Mkuu wa Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Cornel Magembe alisema watuhumiwa huo wanatokea kijiji cha Nyahua Stesheni kilichoko wilayani mwake.

Alisema kuwa Septemba 21, mwaka huu, mabaki ya mwili wa mtendaji huyo yalipatikana na kuthibitishwa kuwa baada ya kuuawa, mwili wake ulichomwa moto.

Akizungumza baada ya kufika nyumbani kwa marehemu katika kijiji cha Mibono Mpya kwa ajili ya kutoa rambirambi ya Sh. milioni tano iliyotolewa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alipofanya ziara mkoani hapa, Magembe alisema tayari hatua zimeanza kuchukuliwa.

Magembe alisema hatua hizo ni pamoja kuchukua majivu kwa ajili ya kuyapeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Alisema kuwa baada ya kupeleka majivu hayo, ilibainika kwamba aliyefariki dunia na mwili wake kuchomwa moto ni Saidi Maduka aliyekuwa ofisa mtendaji wa kijiji.


Alisema watuhimwa hao watafikishwa mahakamani kwa ajili ya kujibu mashtaka yanayowakabili.

Akiwa ziarani mkoani hapa, Dk. Mpango baada ya kupokea taarifa ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, likiwamo tukio hilo, alionesha kusikitishwa na kulitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha watu wote waliofanya mauaji hayo wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

**Ofisa Mtendaji huyo alikutwa amefariki dunia huku mwili wake ukichomwa moto Septemba 9, mwaka huu, ikidaiwa kuwa mauaji yalifanywa wakati anapeleka wito kwa watuhumiwa kufika mahakamani kujibu mashtaka yanayowakabili.**

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# EU yatoa bil. 6.9/- upatikanaji wa nishati safi Tanzania

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

UMOJA wa Nchi za Ulaya (EU) kwa kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Fedha umetoa Euro zaidi ya milioni 2.5 (sawa Sh. 6,986,750,000) kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi na salama inafanikiwa Tanzania.

Mradi huo wa majaribio umeanza kutekelezwa kwenye wilaya 17 zilizoko mikoa sita ikiwamo Mwanza, Tabora, Morogoro, Tanga, Pwani na Dar es Salaam imeanza kuwajengea uwezo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuhakikisha mnyororo wa thamani wa upatikanaji wa nishati safi na salama inafanikiwa nchini.

Ofisa Programu anayesimamia mradi huo kutoka Shirika la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori Duniani (WWF), Makfura Evergris, alisema utaendeshwa kwa miaka mitatu na ukifanya vizuri kwenye mikoa inayofanyiwa majaribio utaenezwa kwenye mikoa mingine nchini.

Evergris alisema hayo kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa wa misitu, waendeshaji wa mashauri kwenye mahakama, mahakimu na maofisa wa Serikali za Mitaa yaliyofanyika mjini Morogoro kwa siku tatu.

Alisema mradi huo umekuja baada ya kufanyika kwa utafiti mwaka 2020 ambao ulionyesha asilimia 63.5 ya Watanzania wanatumia kuni kwa ajili ya kujipatia nishati ya kupikia na kati ya hiyo asilimia 26 wanatumia mkaa kama nishati ya kupikia na kupata joto.

Alisema utafiti huo umeonesha asilimia tano pekee ndio wanatumia gesi na suala la kupata nishati safi ya kupikia bado ni changamoto.

Alisema matumizi ya kuni na mkaa yamesababisha kuangamiza misitu nchini kwa kuwa asilimia 26 ya wanaotumia mkaa inachangia kuwapo kwa tani za mkaa unaotokana na misitu kuvunwa na kuharibu mazingira.

Alisema mradi huo licha ya kuwajengea uwezo TFS, lakini watapatiwa vifaa vya kisasa ikiwamo magari kwaajili ya kufanya doria, radio za mawasiliano, boti za mwendokasi kudhibiti uvushaji wa mkaa kwenye Bahari ya Hindi, ndege nyuki (Drones) kujenga uwezo wa wasimamizi wa Rasilimali za Misitu.

Jaji mstaafu wa Mahakama ya Tanzania, Robert Makaramba, akiwasilisha mada kwenye mafunzo hayo alisema ili nchi iweze kupiga hatua kwenye suala la nishati safi na salama kuna umuhimu wa kupunguza utitiri wa taasisi zinazoshughulikia kila mmoja kipande chake kwenye kuhifadhi misitu na mazingira bila kuwapo kwa mawasiliano.

Alisema ili nchi iweze kusonga mbele kwenye masuala ya kuhifadhi mazingira na nishati safi, zipo taasisi za kuvunjwa na kuziunganisha kuwa moja kwa kuangalia neno la msingi la uhifadhi wa mazingira.

Alitolea mfano nchi ya Ghana ambayo ina kamisheni ya nishati inayoshughulikia nishati zote ikiwamo kuni na mkaa wakati Tanzania ina taasisi nyingi ambazo kila moja inashughulika na kipande chake.

Kuhusu Sheria za Mazingira, Jaji Makaramba alisema ifike wakati mtu akifanya uharibifu wa mazingira asipelekwe jela na badala yake apewe adhabu ya kurudisha aliyoharibu mfano kama amekata mti aende akapande miti 100.

Mratibu wa Asasi ya Kiraia inayojishughulisha na Masuala ya Usimamizi wa Mazingira Tanzania (LEAT), Rajabu Hassan, alisema taasisi hiyo inatekeleza mradi wa mbinu jumuishi za kumaimarisha masuala ya nishati miti ikiwa na lengo la kuzingatia utekelezaji wa sheria za rasilimali za misitu.

Alisema LEAT katika mradi huo itashirikiana na Chuo cha Usimamizi wa Mahakama kwa ajili ya kutengeneza mitaala masuala ya uchunguzi au upelelezi wa makosa ya uhalifu wa misitu yanafundishwa katika vyuo vya elimu ya juu.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akisisitiza jambo wakati akikagua huduma za afya zinazotolewa na Taasisi ya Mafunzo ya Sayansi za afya Haydom, iliyofanyika mwishoni mwa wiki mkoani Manyara. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Iran yaahidi kuendeleza ushirikiano kibiashara Tanzania

**Na Grace Mwakalinga**

IRAN imesema itaendeleza ushirikiano na Tanzania katika nyanja za kibiashara, kisiasa, usanifu wa majengo na sekta ya kilimo hasa cha umwagiliaji, kutokana na uhusiano wa kihistoria uliopo.

Balozi Jamhuri ya Kiislamu ya Iran nchini, Hossein Alvandi Bahineh, alitoa kauli hiyo juzi katika ofisi za ubalozi huo jijini Dar es Salaam, wakati wa ufunguzi wa kituo cha Utamaduni cha Iran na maadhimisho ya Siku ya Washirazi.

Alisema Tanzania na Iran zina uhusiano wa kihistoria ambao unapaswa kulindwa kwa kuwa umekuwapo kwa zaidi ya miaka 1,000, jamii ya Washirazi kutoka Iran walikuja kusini mwa Bara la Afrika hususani katika visiwa vya Zanzibar na maeneo mengine ya pwani ya Afrika Mashariki kwa shughuli mbalimbali ikiwamo biashara.

Alisema ujio wa Washirazi ulikuwa na manufaa kwa sababu ulisaidia kukua kwa biashara, kuimarika kwa siasa nchini na uhusiano wa kidiplomasia uliochangia nchi hizo kubadilishana uzoefu.

"Siku hii muhimu ya ufunguzi wa kituo cha utamaduni wa Iran hapa Tanzania ni kiashiria kuwa tuna ushirikiano mzuri, itasaidia wananchi kujifunza historia ya nchi hizi kabla na baada ya uhuru na mambo yaliyofanyika baina yetu," alisema Balozi Bahineh.

Aliahidi kuendeleza uhusiano huo wa kihistoria kwa kutoa nafasi za mafunzo kwa wataalamu wa Tanzania kwenda kujifunza fani mbalimbali ambazo zinaendeleza na kuenzi uhusiano wa dini, biashara na utamaduni.

"Tunajivunia biashara tuliyonao ya mtindo wa majengo ya Zanzibar pale Stone Town, mtindo wa kilimo cha umwagiliaji na mifumo mingine ya asili ni uthibitisho kuwa Iran na Tanzania ni ndugu wa muda mrefu," alisema Balozi Bahineh. Mkurugenzi wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar, Maryam Mansab, alisema Siku ya Utamaduni wa Washirazi ni muhimu kwa kuwa inatumika kukuza lugha ya Kiswahili ambayo ina maneno mengi ambayo yametoholewa kutoka lugha ya Kishirazi.

Alisema maneno hayo yamesaidia kukuza lugha ya Kiswahili ambayo kwa sasa imeenea duniani na kuwa lugha rasmi katika nchi za Afrika Mashariki.

Ofisa Habari na Uhusiano Bodi ya Huduma za Maktaba nchini, Veronica Bisendo, alisema Iran inasaidia kwa kiasi kikubwa kuandaa vitabu vinavyoonesha historia ya nchi kabla na baada ya uhuru.

Alisema machapisho mengi yapo kwenye maktaba yao ambayo yanaeleza historia ya Washirazi walivyoisaidia nchi kupigania uhuru na kukuza lugha ya Kiswahili, aliwahamasisha wananchi kutembelea maktaba ili kujifunza historia ya Iran.

Miongoni mwa wanafunzi walioshiriki ufunguzi wa kituo cha Utamaduni wa Iran, Latifa Omary, alisema amejifunza kuwa Washirazi ni miongoni mwa waliochangia kutoa maneno yaliyotumika katika lugha ya Kiswahili.

# EPZA yajitanua kiuwekezaji kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) ikiwakilishwa na kikosi maalum cha uhamasishaji uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi kikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, imeongeza wigo wa kuhamasisha uwekezaji kimataifa baada ya kukutana na kufanya maongezi na wawakilishi wa kampuni za China ambazo ni Huaqu International Investment Co. Ltd, na Kampuni ya Global International Promotion Committee.

Kati ya mambo ambayo yalijadiliwa na kufikia makubaliano ilikuwa ni pamoja na kuboresha ushirikiano kwa pande zote mbili ya namna ambavyo taasisi hizi zitaweza kubadilishana taarifa mbalimbali kuhusu fursa za uwekezaji pamoja na kubadilishana uzoefu katika masuala ya kukuza sekta ya viwanda Tanzania.

Ndani ya makubaliano hayo, EPZA itapata ofisi maalum katika Jiji la Shanghai ambayo itarahisisha uhamasishaji na kuwa kiungo kati ya EPZA na kampuni zote za jiji hilo ambazo zitahitaji muongozi katika masuala ya kuwekeza Tanzania.

Katika maongezi haya, EPZA imelenga kupata wawekezaji kutoka China wanaojihusisha na sekta za nguo, ujenzi, usindikaji wa mazao ya kilimo, ngozi, mbao, kahawa, tumbaku na bidhaa za umeme.

Akizungumza na mwandishi, Mkurugenzi Mkuu wa EPZA amedokeza kuwa jitihada hizi ni kutokana na juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akijenga diplomasia ya uchumi ili kuhakikisha kuwa sekta ya uzalishaji inakuwa na bidhaa za Tanzania zinakuwa na soko la uhakika nje ya nchi.

China ni nchi iliyopiga hatua kubwa katika sekta ya viwanda na uzalishaji na hii ni fursa kwa Tanzania kunufaika kwa kuwa kwa sasa nchi hiyo imetenga fedha nyingi kwa ajili ya kampuni yake kuwekeza kimataifa na ni wakati mwafaka kwa Tanzania kuchangamkia fursa hiyo kwa manufaa ya nchi na taifa kwa ujumla.

Katika ziara hiyo Mkurugenzi Mkuu alieleza kuwa viwanda kadhaa vimeonesha nia ya kuwekeza Tanzania ikiwa ni pamoja na cha nguo, bidhaa za ujenzi, kiwanda cha chakula na vifungashio.

EPZA imejipanga kuhakikisha inaendelea na ushawishi wake wa kualika viwanda vingi zaidi ili kutimiza ndoto za Rais ya kuwa na Tanzania ya viwanda ili nchi inufaike na soko huru la Afrika na bidhaa zinazozalishwa katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) kote Afrika zitauzwa katika soko hilo.

Ni wakati wa Tanzania kuimarisha sekta ya uzalishaji kupitia mpango maalum wa kiuchumi wa SEZ ili kunufaika na mikataba mbalimbali ambayo inatiwa saini kimataifa.



# Kamati yaitwisha zigo TCB kulishawishi Bunge

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, imeipa 'kibarua' Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), kulishawishi Bunge kubadili sera na sheria zilizopitwa na wakati, ambazo zinarudisha nyuma maendeleo ya sekta ya kahawa nchini.

Kahawa ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ambayo serikali imeendelea kuyapigia chapuo kutokana na mchango wake wenye tija katika ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Akizungumza katika Mji wa Moshi, Makamu Mwenyeki wa Kamati hiyo, Mariam Mzuzuri, aliitaka TCB kuja na mapendekezo ya kubadili baadhi ya sera na sheria zinazoongoza sekta hiyo.

Aidha, kamati hiyo imeitaka TCB kuhakikisha hoteli zenye hadhi ya nyota mbili hadi tano, zinakuwa na waandaaji wazawa wa kahawa wenye ujuzi, badala ya kutegemea kutumia waandaaji kutoka nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Mzuzuri, kufanya hivyo kutalinda taaluma ya kahawa inayozalishwa hapa nchini na kuleta tija katika sekta hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Primus Kimaryo, akiwasilisha taarifa ya Bodi ya Kahawa Tanzania kwa kamati hiyo, alisema kwa mwaka 2024, menejimenti yake imepanga kuzalisha miche bora ya kahawa 22,628,919 sawa na asilimia 113.1 ya lengo lililowekwa la kuzalisha miche milioni 20 na kuisambaza kwa wakulima.

Katika mpango wa kuimarisha uzalishaji wa zao hilo, Kimaryo alisema TCB inatekeleza mradi wa uchimbaji wa visima 10 kwa ajili ya umwagiliaji kwenye mashamba ya kahawa ya Mbozi, mkoani Songwe.

"Malengo yetu ni kuimarisha pia mashamba makubwa ya hekta 4,000, ambapo kati ya hizo, eneo lenye ukubwa wa hekta 358 limepatikana Wilaya ya Karagwe, Kagera," alieleza.

Alisema mfumo wa masoko wa Direct Export, umeisaidia Tanzania kuuza kahawa nje ya nchi kwa asilimia 80.

# China, Tanzania kushirikiana ujenzi wa makumbusho

**Na Godfrey Mushi,** KARATU

CHINA na Tanzania zimeanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa makumbusho ya jiolojia ya Ngorongoro-Lengai katika Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, unaogharimu Sh. bilioni 25.

Mradi huo unalenga zaidi kuendeleza maeneo ya kale ambayo yanahifadhi jiolojia na kukuza utalii wa miamba, miti na wanyama.

Akizungumza katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi mradi huo, unaofadhiliwa na Serikali ya Watu wa China, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema jengo hilo ni mahususi kwa ajili ya uhifadhi wa utalii wa miamba au jiolojia inayohusisha matumizi ya eneo la jiografia lenye umuhimu wa kisayansi, utamaduni wa kihistoria.

"Jengo hili la Makumbusho ya Ngorongoro-Lengai UNESCO Global Geopark linaakisi mila na desturi zetu, hasa nyumba za jamii ya wafugaji wa kimasai. Lakini linaakisi Ngorongoro Kreta kama ilivyokaa.

...Maeneo ya utalii huu wa miamba, utalii wa jiolojia yanajumuisha milima, maziwa na mandhari mengine ya asili. Maeneo ya Jiopark upande huu ni Olduvai Gorge, Kreta ya Ngorongoro, Mlima Oldonyo Lengai, nyayo za Laitoli na miti maalumu; maeneo ambayo Watanzania tumeendelea kuyalinda na kuyatumia ipasavyo. Wananchi wetu wakati mwingine wanafanya matambiko katika maeneo haya."

Balozi wa China hapa nchini, Chen Mingjian, akizungumzia mradi huo alisema, serikali ya nchi hiyo itaisaidia Tanzania kuzalisha mapato ya Dola za Marekani bilioni sita kutokana na sekta ya utalii.

Aidha alisema makumbusho hayo yataisaidia Tanzania kufikia lengo lake la kutembelewa na watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025.

"Juhudi za China kutangaza utalii wa Tanzania, hasa kupitia Filamu ya Tanzania Amazing iliyotengenezwa kwa ushirikiano wa Kim Dong, mwigizaji maarufu wa China ambaye ni balozi wa utangazaji wa utamaduni na utalii, kati ya nchi hizo mbili," alisema Balozi Mingjian.

Kazidata ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), inaonyesha hadi kufikia mwezi Julai mwaka huu, idadi ya watalii waliowasili nchini ilikuwa 2,026, 378. Pengo la watalii lililopo kwa sasa ili kufikia idadi hiyo ni watalii 2,973, 622 ili kufikia lengo hilo la mwaka 2025.

Meneja mradi huo kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Dk. Agness Digna, alisema mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza, inahusisha masuala ya ufundi, kwa wataalam kuingia kutafuta taarifa mbalimbali za maeneo hayo.

Alisema kwa sasa wataalamu wanadadisi kwenye eneo hilo kuna nini ili waweze kuandika taarifa hizo vizuri na kuweka katika mabango kwa ajili ya watalii kuona, kujifunza.

"Kwa mfano maeneo ya kreta, ukipita utaona jinsi gani kreta imetengenezwa miaka milioni mbili iliyopita. Kwa hiyo awamu hiyo ilihusu utafiti wa hayo maeneo. Tulianza Juni 2020 na itakamilika Mei 2025, taarifa nyingi tumeziweka kwenye maeneo mbalimbali.

Kamishna wa NCAA, Dk. Elirehema Doriye, alisema mradi huo utawainua kiuchumi na kuongeza ajira kwa wananchi wa Wilaya za Karatu, Ngorongoro, Monduli na Longido kwa kutoa fursa za kiuchumi kupitia utalii wa miamba.



Ofisa Ushirika Mwandamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Ndimolwo Laizer, akiwajengea uwezo viongozi na jamii katika Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, kuhusu kujiunga na ushirika kwenye kikao kilichofanyika mji mdogo wa Orkesumet juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mchakato kutokomeza magonjwa ya mifugo waanza

**Na Allan Isack,** LONGIDO

SERIKALI wilayani Longido mkoani Arusha imeendelea na mchakato wa kupambana na kudhibiti magonjwa mbalimbali yanayoshambulia mifugo, ikiwamo ugonjwa wa ndigana baridi.

Serikali imefikia hatua hiyo kutokana na magonjwa hayo kuathiri mifugo ikiwamo ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda katika eneo hilo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Mutallah Mbillu, alieleza hayo juzi wakati akiongoza zoezi la kuogesha mifugo katika eneo la Lata lililopo Kata ya Oloipiri wilayani humo.

Mkurugenzi huyo, alisema zoezi hilo limetekelezwa ukiwa ni mkakati wa kuimarisha ufugaji kwa wafugaji kufuga kwa tija.

Alisema katika kusaidia utekelezwaji wa mpango huo, ametoa msaada wa lita 12 za dawa ya kuogesha mifugo, ambayo itawawezesha wananchi kuogesha mifugo yao bure.

Hata hivyo, Mbillu, aliwataka wafugaji kuogesha mifugo yao kila baada ya siku saba badala ya desturi ya kuogesha kila mwisho wa mwezi, ili kuhakikisha kinga madhubuti dhidi ya ndigana baridi.

Aidha, alisema kuwa afya bora ya mifugo ni muhimu kwa ustawi wa kiuchumi wa halmashauri hiyo kwa kuwa wafugaji ni nguzo kuu ya mapato ya halmashauri hiyo.


Ofisa Kilimo, Mifugo, na Uvuvi wa Halmashauri hiyo, Chobby Chubwa, alisema wamekuwa wakiwahimiza wafugaji kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo.

Kadhalika, alisema ugonjwa wa ndigana baridi unaweza kudhibitiwa kwa njia ya kuogesha mara kwa mara.

Ofisa huyo wa mifugo, alisema asilimia 70 ya magonjwa ya mifugo hutokana na kupe, hivyo kuogesha mifugo ni hatua muhimu katika kuboresha afya ya mifugo.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji wilayani humo, Ramatho Saringe, mkazi wa Kijiji cha Oloipiri, aliishukuru serikali kupitia halmashauri kwa kuanzisha na kusimamia zoezi hilo.

Alisema zoezi la uogeshaji wa mifugo ni hatua muhimu kuwa itasaidia kudhibiti ugonjwa wa ndigana baridi ambao umekuwa changamoto kubwa kwa mifugo yao.



# Wakulima vijana wawaita maofisa ugani shambani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA hususani vijana katika Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamewataka maofisa ugani kutoka ofisini na kuwafikia vijijini kuwaelimisha namna ya kulima kisasa.

Wamesema lengo ni kuweza kuzitumia vema pembejeo wanazopewa bure na serikali kila mwaka ili kupata mazao mengi na kujiinua kiuchumi.

Hayo yalibainishwa juzi na baadhi ya vijana 59 kutoka kata 12 kati ya 20 za halmashauri hiyo wakati wakikabidhiwa pembejeo za Sh. milioni 75.916 na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita kwa ajili ya kilimo cha msimu wa 2024/25.

Mmoja wa vijana hao, Chausiku Clement kutoka Kata ya Mwendakulima alisema ili kuzalisha mazao ya chakula, biashara na mikunde ni vema wakatembelewa na maofisa ugani mashambani na kupewa elimu namna ya kulima kisasa.

Alisema wamekuwa wakilima mashamba makubwa zaidi ya hekari tano lakini mavuno wanapata kidogo hasa katika mazao ya mahindi, pamba na alizeti.

Naye Alfred Masanja alisema kilimo cha kisasa kitasaidia kuwa na manufaa makubwa wakitumia wataalamu, kwamba hata zile dhana za kishirikina wanapofeli kupata mavuno ya kutosha kuwa wamerogwa hazitakuwapo.

Kaimu Ofisa Kilimo Manispaa hiyo, Pendo Matulanya, alisema, jumla ya mifuko 594 ya mbolea za kupandia, kukuzia, viwatilifu lita 18, mbegu za mahindi na alizeti zenye uzito wa kg 50 zimetolewa kwa vijana hao.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, aliwataka maofisa kilimo wa ngazi za kata kuhakikisha wanawasimamia vema katika kuwaelimisha wakulima kulima kisasa.

Alisema vipindi vya kuweka mbolea na viuatilifu ili mashamba yao yaweze kuleta tija katika uzalishaji na lengo la serikali la kumkomboa kijana katika sekta ya ajira ili liweze kutimia.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, na Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Kahama, Abdul Mpei, wakipanda mti katika eneo la ujenzi wa kituo cha polisi kata ya Busoka, kinachojengwa kwa nguvu ya wananchi pamoja na wafanyabiashara kwa lengo la kukabiliana na uhalifu wa mali zao jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# NeST yatajwa kukwamisha miradi ya maendeleo

**Na Daniel Limbe,** BIHARAMULO

MFUMO wa Kielektroniki wa Manunuzi ya Umma nchini (NeST) umedaiwa kikwazo cha kutokamilika kwa baadhi ya miradi ya maendeleo yenye ubia na nguvu za wananchi.

Mapendekezo hayo yametolewa juzi kwa nyakati tofauti na madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera wakati wakiwasilisha taarifa za maendeleo ya kata zao kwenye kikao cha robo ya kwanza.

Pamoja na mambo mengine walisema mfumo huo huenda ukawa mzuri mazingira ya mijini ukilinganisha na vijijini, kwamba baadhi ya mapendekezo yakitaka mfumo huo ufutwe.

"Huu mfumo wa NeST umekuwa ukituletea watu ambao ni wageni kabisa mazingira yetu na baadhi yao wanapokuja eneo la mradi wakagundua na kuona baadhi ya vifaa vya ujenzi vinapatikana mbali hivyo kutelekeza mradi," alisema Diwani wa Kata ya Runazi, Aniceth Bruno.

Aidha alisema ipo miradi iliyokuwa inachangiwa fedha kwa nguvu za wananchi na pesa hizo zilipaswa kupitia kwenye akaunti za vijiji kabla ya kutumika, lakini miradi mingi yenye ubia huo imesimama baada ya mafundi kutolipwa fedha kutokana na mfumo huo wa NeST kugoma kuruhusu pesa kwa zaidi ya miezi tisa.

Alitaja baadhi ya miradi iliyokwama kutokana na mfumo huo kuwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa matundu ya vyoo vya shule pamoja na ujenzi wa zahanati.

Diwani wa Kata ya Biharamulo, David Mwenenkundwa, alionyesha mashaka juu ya ukuzaji wa mafundi wa ndani kupitia mfumo wa NeST na kuwa baadhi yao wanashindwa kujiunga na mfumo kwa sababu ya gharama kubwa zilizowekwa ikiwamo Sh. 80,000 ya kujisajili, Sh. 100,000 kwa ajili ya leseni.

Gharama zingine ni Sh. 10,000 kwa ajili ya kuomba zabuni pamoja na makadirio ya Mamlaka ya Mapato nchini (TRA).

Diwani wa Kata ya Ruziba, Athanas Sumbuso, alisema ipo hatari kubwa ya saruji zilizotolewa na mfuko wa jimbo hilo kwenye baadhi ya vijiji vyenye miradi ya ujenzi kuganda kutokana na mfumo wa NeST kutoruhusu fedha kutumika, hali inayoweza kusababisha hasara kubwa kwa miradi hiyo.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Innocent Mkandara, mbali na kukiri juu ya miradi kushindwa kuendelea na ujenzi, alisema jitihada zinafanyika kwa kutoa elimu kwa jamii, wazabuni, makandarasi, mafundi wa ujenzi wasio na mitaji pamoja na watendaji wa vijiji na kata ili kutumia mfumo huo kwa kuwa ndiyo maelekezo ya serikali.

Alisema: "Changamoto nyingine kwa baadhi ya wadau wetu waliojiunga kwenye mfumo ni kutopata taarifa za zabuni zilizotangazwa ila tunampango mzuri wa kuwajulisha kwa simu kila tutakapotangaza ili waingie kwenye mfumo kuomba kazi hizo".

# CHADEMA yalia wagombea wao 400 kuenguliwa

**Na Samsom Chacha,** TARIME

VIONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wilayani Tarime mkoani Mara, wamelaani hatua ya wagombea wao zaidi ya 400 kuenguliwa katika kinyang'anyiro cha kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Wamesema hatua hiyo ni ishara ya kuvuruga uchaguzi, kuiomba mamlaka husika kutatua haraka tatizo hilo.

Katibu Mwenezi wa chama hicho, Jimbo la Tarime Vijijini, Mrimi Zabron alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari akisema wagombea 400 wameenguliwa kwa sababu zisizo na msingi.

Alisema kati ya wagombea hao wajumbe kundi la wanawake ni 280, wenyeviti wa vitongoji 150 na wenyeviti wa vijiji watano.

Zabron alisema waliweka wagombea vijiji vyote na waliwekewa pingamizi vijiji 13 na wameenguliwa wagombea wa vijiji vitano vya mpakani Sirari.

Akitolea mfano, Zabron alisema mgombea Nyango Paulo aliengüliwa kwa madai kuwa uraia wake unautata, wakati miaka ya nyuma aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji hicho kwa miaka 10 na diwani kata ya hiyo kati ya mwaka 2015/20.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Tarime, Mwita Isasi, alisema kamati ya rufani iliyokuwa inasikiliza mapingamizi haikuwatendea haki wagombea wao na kuiomba serikali kuwachia wananchi mchakato huo ili kupata viongozi wanaowataka.

Juzi, katika taarifa yake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa alisema wote walioenguliwa ni kwa mujibu wa kanuni na sheria na uchaguzi ni kanuni wala siyo huruma.

Mchengerwa alikiri kuwepo kwa mikoa ambayo wagombea wake hawakuwa raia wa Tanzania ikiwamo Lindi, Kigoma na Rukwa.



Ukurasa 12



NDANI YA COP29...
Mafuriko, vimbunga ni shida wakati joto na jua kali ni balaa likichoma Dar

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 19, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14
Zanzibar ni darasa mataifa kujifunza pensheni kwa wazee

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

GHOROFA KARIAKOO

# Mtaalamu ataka majumba yahakikiwe kujua uimara, uduni na uhimilivu

ILI kutibu ghorofa za Kariakoo Dar es Salaam, zinazoporomoka mara kwa mara na kuua, wadau wameungana na serikali kutaka kufanyika uhakiki wa uimara na uhimilivu wa majengo hayo.

Hadi sasa idadi ya waliopoteza maisha katika ajali hiyo ya mwishoni mwa wiki iliyotokea Jumamosi ni 13. Aidha, majeruhi ni 84 huku wengine 26 wakiokolewa, Rais Samia Suluhu Hassan anasema, akiwa Brazil kwenye mkutano wa mataifa tajiri zaidi G20.

Itakumbukwa kuwa ni tukio linalotokea miaka miwili baada ya watu watano kufariki dunia na 17 kujeruhiwa wakati jengo la ghorofa lilipoporomoka Goba kwa Awadhi Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa lilikuwa linajengwa na kuongezewa ghorofa nyingine juu bila kuimarisha msingi. Ni mkasa uliotokea Desemba 2021 jengo hilo likiangukia nyumba za jirani na kusababisha maafa kwa watu na mali zao.

Kisa cha Goba kinatanguliwa na kingine kilichotokea katikati ya Dar es Salaam, miaka 11 iliyopita nacho ni kubomoka kwa ghorofa lililokuwa linajengwa kwenye makutano ya mitaa ya Indira Ghandi na Zanaki.

Katika matukio hayo watu wamepoteza maisha na sasa kuna haja ya kuchukua hatua za kitaalamu kuhakiki uimara na kutibu majengo duni yanayoua watu, kama anavyosema Rais Samia.

Akimuunga mkono Rais, Sebastian Moshi, msanifu majengo na mkandarasi ujenzi, anasema anachosema Rais ni muhimu.

Anakumbusha kuwa baadhi ya majengo Kariakoo yamejengwa 'kijanja'.

Anasema kama mmiliki amekwepa kutumia mkandarasi ambaye ni mshauri wa kitaalamu na ndiye mtekelezaji wa ujenzi kusimamia kazi maafa kama hayo hayakwepeki. Mtaalamu huyo wa ujenzi na mchora majengo, anaeleza kuwa ni lazima kufanya ujenzi kwa misingi ya kitaalamu la sivyo hatari zitatokea zaidi.

Anasema kufuatia maelekezo ya Rais, serikali iwaagize wenye ghorofa kugharamia kupima uimara na uhimilivu wa majengo yao.

Kinachotakiwa kufanyika ni pamoja na kutindua na kufukua maeneo muhimu kwenye majengo hayo kama mihimili (columns) na kupima mzigo unaobebwa na jengo yaani maduka na bidhaa zake.

Kadhalika anataja kukagua zege, matofali, nondo na vyuma vilivyotumiwa, uimara wa msingi wa majengo hayo vyote vichunguzwe kwa gharama za wamiliki.

Anasema ni jambo ambalo linaweza kufanyika serikali ikiamua na sasa imeonyesha dhamira.

"Wahandisi majengo wapo ambao wanaweza kupewa jukumu hilo, kampuni binafsi za ujenzi zipewe kazi hiyo pamoja na vitendeakazi vya kukamilisha uchunguzi kwa wakati."

Anasema ni lazima wafanyabiashara wahakikishiwe usalama wao kutokana na matukio hayo kujirudia.



Askari wa uokoaji wakiendelea kuwatafuta watu kwenye ghorofa lililoanguka mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: IMANI NATHANIE**

### KUCHUKUA HATUA

Moshi anakumbusha kuwa ili kuwa na ujenzi madhubuti kunahitajika jicho la mhandisi mchora majengo ili kupata ramani.

Aidha anamtaja mhandisi wa mihimili, huyu anaangalia mifumo na uimara wa mihimili na jicho la tatu ni la mkadiriaji majenzi anayeangalia 'matirio' na kuhakikisha kuwa yana viwango vinavyohitajika.

Moshi anafafanua kuwa baada ya ramani, anayekadiria majenzi anaanzia nondo, matofali, mchanga, chuma, mawe, kokoto na kila kitu kinachohitajika kwenye ujenzi na kuthibitisha ubora wake.

Anasema viwango na uimara ni muhimu ili kuliongezea umadhubuti na uhimilivu kuepusha matukio kama hayo.

### CHANZO AJALI

Akizungumzia kinachoweza kuwa chanzo cha kuporomoka jengo hilo lenye ghorofa nne anasema sababu kubwa huenda ni kukosekana usimamizi wa kitaalamu baada ya kuanza ujenzi.

Moshi anafafanua kwamba ujenzi wa ghorofa unapoanza ni lazima wawepo wataalamu au wahandisi wajenzi kufuatilia na kusimamia kuwa kila hatua na kila kinachohitajika kinafanyika kama kilivyoelekezwa kitaalamu.

Kwa mfano, anasema ili kazi hizo zifanyike kwa misingi inayokubalika kihandishi na kisheria, mmiliki anapopewa kibali cha ujenzi ni lazima bodi za wahandisi ziidhinishe mtaalamu anayesimamia na awe amesajiliwa na bodi hizo.

Baadhi ya bodi zinazowasajili wahandisi zinazoidhinisha kazi za ujenzi wa majengo ni pamoja na ile ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) na ile ya Usajili wa Wahandisi (ERB).

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA GAUDENSIA
MNGUMI

MABADILIKO TABIANCHI KITISHO KISICHOJALI MASKINI, MATAJIRI

# Mafuriko, vimbunga ni shida wakati joto na jua kali ni balaa likichoma Dar na mikoani pia

MKUTANO wa mwaka huu wa Umoja wa Mataifa kuhusu tabianchi (COP29), umeanza Jumatatu iliyopita huko Baku, Azerbaijan, ukitarajiwa kuhitimishwa Ijumaa wiki hii.

Ukiwaleta pamoja viongozi wa nchi, wafanyabiashara na AZAKI unasaka majawabu dhidi ya ongezeko la joto duniani linalotishia hatima ya binadamu na viumbe wengine baada ya fukuto na joto kali kuvunja rekodi mwaka huu.

Pengine kuna Watanzania ambao hupuuza au hawafahamu ukweli kuhusu mabadiliko ya tabianchi na huchukulia suala hilo kama vile haliwahusu. Tatizo lipo na hata leo wafungue macho walione.

Joto limeongezeka na jua ni kali mno ukanda wa pwani kuanzia Tanga hadi Mtwara, Unguja na Pemba, Mafia na pia theluji ya Mlima Kilimanjaro inazidi kuondoka, huku mkoa huo ukiwa na joto kali likifikia nyuzi 33 kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa.

Afrika na Tanzania si mchangiaji wa ongezeko la joto duniani linalotokana na uzalishaji wa kiwango kikubwa cha hewa chafuzi ya karboni ambayo imejaa angani.

Hewa hiyo inaondoa utando wa tabaka linalozuia mionzi mikali ya juu kufika duniani kwa wingi na haraka. Tabaka hilo la 'ozoni' linayeyushwa na joto kutoka hewa chafuzi hasa karboni (hewa ukaa )na kuchochea mabadiliko ya tabianchi.

Mabadiliko hayo huongeza joto, upepo, mvua kupindukia, vimbunga na tufani. Kwa mfano Kimbunga Hidaya kilitikisa Pwani ya Afrika Mashariki.

Mei mwaka huu kilishuhudiwa kisiwani Mafia, Mikoa ya Lindi na Mtwara kikivuruga na kutishia maisha, vyombo vya habari vikiripoti kuwa nyumba zaidi ya 50 zilivunjwa Mafia na kimbunga hicho, huku mamia ya wananchi wakipoteza mali kuanzia mazao mashamba, mifugo na biashara.

Kimbunga 'Keneth' karibuni kiliivuruga Msumbiji bila kusahau mwaka 2019 kimbungai 'Idai' kilisababisha maafa ukanda wote wa Kusini mwa Afika kuanzia Malawi, Zambia, Zimbabwe na Msumbiji.

Hata leo ukanda huo unakabiliwa na ukame kutokana na ukosefu wa mvua wa miaka kadhaa.



Kimbunga Hidaya kilivyosababisha maafa na kubomoa barabara mkoani Lindi, tufani pia ikiharibu maisha na mali nchini Msumbiji. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Tutaweza kupata msaada wa moja kwa moja kwa mahitaji yetu maalum, ikiwamo ushauri wa kisaikolojia na vifaa vya kisasa vya teknolojia vya kujifunza.

Baadhi ya mataifa ikiwamo Zambia yanategemea mahindi kutoka Tanzania.

Kuanzia mwezi uliopita nchini Nigeria mafuriko makubwa yametikisa taifa hilo kwa zaidi ya mwezi jimbo la Kogi, Borno na mji mkuu Maiduguri liliathiriwa na mamilioni ya watu kukosa makazi, inasema BBC Swahili.

Kwa upande mwingine mwaka 2022 nchi za Kusini mwa Afrika ziliathiriwa na dhoruba ya kimbunga 'Ana' ambacho kilikuja na upepo mkali, mvua kubwa na kufanya uharibifu pamoja na kusababisha watu wengi kupoteza maisha, kubomoa miundombinu, makazi, mashamba na kuvuruga uzalishaji, usambazaji na upatikanaji nishati.

Mataifa mfano Madagascar kwa mujibu wa takwimu za serikali hiyo Januari 2022, takriban watu 131,000 waliathiriwa na kimbunga Ana nchini humo ikiwa ni pamoja na wengine 71,000 kuyakimbia makazi yao, na kuua watu 58 karibu wote wakiwa katika mji mkuu wa Antananarivo ambako nyumba za asilii zilibomoka na kufukiwa wengine wakisombwa na kufukiwa na maporomoko ya ardhi.

Hata leo hali ni ngumu nchini Sudan Kusini, mafuriko yanatikisa na huko watu 893,000 wameathiriwa na zaidi ya watu 241,000 wameyakimbia makazi yao, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Kibinadamu (OCHA), inaripoti mwezi uliopita.

Ni dhahiri watu duniani kote wanaathiriwa vibaya na matukio ya kutisha ya hali ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Leo mkutano wa COP 29, unapoendelea huko Azerbaijan iliyokuwa sehemu ya Urusi kabla ya kusambaratika Umoja wa Kisovieti, kinachomulikwa zaidi ni kupata fedha za kukabiliana na athari hizo hizo.

Zinahitajika fedha wakati huu ambao matrilioni ya dola yanatakiwa kupunguza kwa kiwango kikubwa hewa chafu na wakati huo huo kulinda maisha na mbinu za kujipatia kipato ili visisambaratishwe na mabadiliko ya tabianchi.

Mkutano huo unatoa fursa kwa nchi kuwasilisha mipango yao ya kitaifa iliyoboreshwa ya jinsi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kwa mujibu wa Mkataba wa Paris wa mabadiliko ya tabianchi, mipango ambayo inatakiwa iwe imekamilishwa ifikapo mwaka 2025.

Taarifa za Mtandao wa UN News, zinaeleza kuwa Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Mkataba wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), Simon Stiell, wakati anafungua mkutano wa 29 wa nchi wanachama wa mkataba huo, anauliza maswali mengi.

Kwa mfano, anawauliza wajumbe mnataka bei za vyakula na nishati ziongezeke zaidi? Mnataka nchi zenu ziendelee kushindwa kushindana kiuchumi? Je, mnataka dunia yetu iendelee kukosa utulivu na kugharimu maisha adhimu ya binadamu?

Stiell anahoji maswali hayo kwa kufuatia mwaka mwingine wa viwango vya juu vya joto kali na matukio ya kupitiliza ya hali ya hewa mbaya duniani kuanzia mafuriko, ukame na dhoruba kali ambapo anasema malengo mapya ya ufadhili kwa tabianchi ni muhimu kwa ajili ya ustawi wa mataifa, yakiwamo tajiri na yenye uthabiti.

Anawaambia washiriki wa mkutano huo ulioanza wiki iliyopita ukitarajiwa kumalizika Ijumaa Novemba 22, kwamba kwa kadri madhara ya mabadiliko ya tabianchi yalivyo dhahiri ni lazima kukubaliana mwelekeo mpya wa kufanikisha kupata fedha za kugharamia miradi ya kukabili na kuhimili.

Mkutano wa Baku unataka nchi kuanzisha lengo jipya la ufadhili kila mwaka kwenye miradi ya tabianchi kuchukua nafasi ya ahadi yam waka 2009 ya dola bilioni 100 kila mwaka, mpango unaomaliza muda wake mwishoni mwa mwaka huu, na ambalo washirika wanasema ni lengo la chini kwa mujibu wa kile kinachohitajika kukabili ongezeko la viwango vya joto angani, duniani na baharini.

Stiell anasisitiza kuwa mchakato wa UNFCC ndiyo pekee ambao unaweza kutatua janga la tabianchi lililosambaa duniani kote, na kuwezesha kuwajibisha wachafuzi.

"Na tunafahamu mchakato huu unafanya kazi.Kwa sababu bila ya kuwapo kwake, dunia ingekuwa inaelekea kwenye ongezeko la joto duniani la nyuzi joto tano."

Anawaambia washiriki kuwa hakuna taifa lililo na kinga dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na pia akatoa mifano ya mafanikio na kuelezea makubaliano mapya ya ufadhili wa fedha kwa changamoto za tabianchi ni muhimu.

Anasema kila nchi itaathirika iwapo theluthi mbili ya nchi duniani hazitaweza kupunguza kwa kasi kubwa utoaji wa hewa chafuzi.

Halikadhalika, uchumi wa dunia nzima utaporomoka iwapo nchi hazitaweza kuimarisha mnyororo wao wa usambazaji wa bidhaa wakati huu wa ongezeko la gharama unaohusishwa na changamoto za tabianchi, kama vile kupungua kwa kina cha maji kwenye Mfereji wa Panama, jambo ambalo limepunguza idadi ya meli zinazosafiri kupitia eneo hilo.

Anaeleza kuwa muongo wa 2015 hadi 2024, umevunja rekodi ya kiwango cha joto linasema Shirika la Umoja wa Mataifa la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

COP29 ikifungua pazia la WMO imetoa ripoti yake ya hali ya hewa duniani kwa mwaka huu wa 2024, ikiweka bayana tahadhari kutokana na kasi kubwa ya mabadiliko ya tabianchi ndani ya kizazi kimoja, ikichochewa na ongezeko la hewa chafuzi angani.

Miaka ya kuanzia 2015 hadi 2023 inabaki kuwa muongo uliovunja rekodi kwa kuwa na viwango vya juu vya joto, inasema WMO.

Inasema sambamba na theluji baharini zikiyeyuka, kina cha maji ya bahari kikiongezeka, halikadhalika joto la maji ya bahari linaongezeka pia.

Hali ya joto kali au baridi kupindukia inavuruga maisha ya watu na uchumi duniani kote.

Ripoti inasema kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu, wastani wa joto angani ulikuwa nyuzi 1.54 zaidi ya kiwango cha kabla ya mapinduzi ya viwanda, ukichochewa na mkondo joto wa maji baharini, El Niño.

Takwimu hizo ni kutoka vituo sita vya kimataifa vya kufuatilia hali ya hewa duniani ambavyo hutumiwa na WMO, kiama cha tabianchi kinatishia huduma za afya, kinachochea ukosefu wa usawa, kinakwamisha maendeleo endelevu na kutikisa amani.

Wale walio hatarini zaidi ndio wameathiriwa vibaya zaidi," anasema Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres kwenye utangulizi wa ripoti hiyo.

### KWENYE HATIHATI

Mkuu wa UNFCCC Simon Stiell, anatoka Grenada ambako kisiwa chake cha Carricou kilikaribia kuzama Julai mwaka huu baada ya kupigwa na kimbunga Beryl.

Akizungumza wakati picha za uharibifu wa kisiwa hicho zikiwa nyuma yake, Stiell anawaambia washiriki wa COP29 kwamba alitiwa moyo na wananchi wenzake ambao pamoja na kuathiriwa na vimbunga vitokanavyo na mabadiliko ya tabianchi, wameamka tena na tena na kuendelea kupambana.

Anamalizia hotuba yake kwa kukumbusha wajumbe kuwa COP29 ni ya kihistoria hivyo, "hatuwezi kuondoka Baku bila matokeo ya dhati,"anasema akitoa changamoto kwa wajumbe "kusimama kidete na kuleta matokeo."




Tufani iliharibu maisha na mali nchini Kenya.

### AFRIKA IBADILIKE

Afrika inaumizwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi kama ongezeko la joto ambalo linatishia kilimo, maji na uzalishaji karibu sekta zote lakini inawajibika kikamilifu kukabiliana hali hiyo?

Bara hilo ni ukanda wa tufani na vimbunga ni lazima lijue kuwa hakuna wakuisaidia kikamilifu hasa wahisani ambao miongoni mwao ni wazalishaji wa hewa chafuzi.

Ripoti za kimtandao zinaeleza kuwa hadi kufikia 2022, mataifa matano wazalishaji wakubwa wa hewa au gesi chafuzi ni China, Marekani, India, Russia na Japan. Afrika inachangia kiasi kidogo cha hewa chafuzi ambayo ni chini ya asilimia tatu.

Hata hivyo, baadhi ya ajenda ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinaonyesha kuwa hazilengi kuisaidia Afrika bali kuwanufaisha wahisani wanaotoa fedha zao.

Kwa mfano fedha zinaelekezwa kwenye semina, mikutano na makongamano lakini hakuna jambo linalofanyika kwenye sehemu zinazoathirika.

Kwa kifupi hakuna suala ambalo ni endelevu kwa upande wa Afrika, ikimbukwe semina na mikutano siyo jambo endelevu, linalotatua changamoto kwa mfano mafuriko kwenye makazi.

> Na tunafahamu mchakato huu unafanya kazi.Kwa sababu bila ya kuwapo kwake, dunia ingekuwa inaelekea kwenye ongezeko la joto duniani la nyuzi joto tano.

Watu wanazungumzia fedha za kuvuna kaboni kwenye baadhi ya vijiji zinafanywa kwa maelekezo ya wataalamu wa nchi wahisani ndiyo wanaokadiria na kupanga malipo pamoja na gharama zote, wengine hawahusiki.

Pengine hakuna kubwa la kutegemea kutoka Azerbaijan mbali na wajumbe wa nchi za Afrika kwenda kufanya 'shopping'. Lazima kuanzia sasa wabadilike kila nchi iwe na mikakati halisi inayofungama na mipango ya maendeleo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Afrika ijitazame kwa sababu bado matumizi ya serikali zake ni makubwa zinatumia, magari ya kifahari, kulipana mishahara minono na posho kubwa iwekeze kununua ndege za uokoaji wakati wa mafuriko, iwe na vifaa vya kisasa vya uokozi. Aidha iimarishe mifumo ya kutambua na kuchukua tahadhari kabla ya maafa hasa vimbunga, tufani, kukosa maji, ukame na njaa.

Lazima ijitafutie akiba ya fedha kukabiliana na majanga na mbadala wa kuwekaza kwenye mabadiliko ya tabianchi kwa juhudi zao wenyewe na kutumia jukwaa la COPs kujizatiti badala ya kuamini kuwa mataifa yaliyoendelea yatawapa fedha kukabili tatizo hilo.

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Zanzibar ni darasa mataifa kujifunza pensheni kwa wazee

• Wamo wanafunzi kutoka Rwanda, Uganda, Kenya

MIAKA nane sasa wazee wa Zanzibar waliofikisha miaka 70 na kuendelea wanapata pensheni ya kujikimu ambayo hutolewa kila mwisho wa mwezi, ikijulikana kama pensheni jamii.

Zanzibar ni ya kwanza Afrika Mashariki kutoa pensheni jamii kwa wazee na nchi mbalimbali za Afrika Mashariki zinafika visiwani humo kujifunza namna ilivyofanikiwa kutoa fedha kwa wazee.

Baadhi ya wanafunzi waliokuja kusoma ni kutoka Kenya, Uganda na Rwanda.Uamuzi wa kutunza wazee ulianza miaka nane iliyopita na awamu ya Dk. Ali Muhamed Shein, akiwapa wazee Sh. 20,000 kwa kila aliyefikisha miaka 70 na kuendelea.

Katika uongozi wa miaka minne ya Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameendelea kuwajali wazee, akienda mbali zaidi kwa kuongeza kiwango cha pensheni jamii kutoka Shilingi 20,000 hadi 50,000. Kiwango hicho cha fedha kwa sasa kinatolewa kwa wazee 30,552 kati ya hao Unguja 18,105 na Pemba 12,447 waliosajiliwa ndani ya mpango huo.

Maono ya viongozi hao yanatokana na matamanio ya mwasisi wa Zanzibar Mzee Abeid Amani Karume ambaye ni kielelezo cha kuwajali na kuwaenzi wazee ambao tangu mwaka 1964 baada ya Mapinduzi hadi sasa wanalelewa katika nyumba maalum za serikali Unguja na Pemba.

Serikali ya Dk. Mwinyi inaendeleza jitihada za kuwahudumia na kuwatunza wazee wasio na ndugu wala jamaa katika makao maalum yaliyopo Sebuleni, Welezo kwa Unguja na Limbani kwa upande wa Pemba na jumla ya wazee 68 wanatunzwa katika maeneo hayo yaliyoanzishwa na Mzee Karume.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma. **PICHA: MTANDAO**

Mchanganuo wa wazee hao kati ya 68, wazee 38 wapo Welezo wakiwamo wanawake 13 na wanaume 25, Sebuleni 21 wanawake 13 na wanaume wanane kwa Unguja na kwa Pemba Limbani wapo wazee tisa wanawake watatu na wanaume sita. Wote wanaendelea kupatiwa huduma za kiustawi ikiwamo chakula, mavazi, malazi, matibabu na fedha za kujikimu.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, anasema serikali kwa kuona umuhimu na mchango mkubwa wa wazee katika kuleta maendeleo ya nchi iliongeza kiwango hicho cha pensheni jamii kutoka 20,000 hadi 50,000 sawa na asilima 150.

Anasema hatua hiyo ni miongoni mwa utekelezaji wa sera ya hifadhi ya jamii ya mwaka 2014 ambayo inaeleza changamoto kubwa inayowakabili wazee ni ukosefu wa usalama wa kipato.

"Pensheni hii inawasaidia wazee kuimarisha maisha yao, ikiwamo kuanzisha shughuli mbalimbali za kujipatia kipato. Kuumarisha zaidi mpango huu, serikali imeandaa sheria ya kusimamia masuala ya wazee namba mbili ya mwaka 2020," anasema Waziri.

Anasema sheria hiyo imeweka miongozo imara inayohakikisha wazee wanapatiwa pensheni kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na serikali inafanya kila juhudi kwa kushirikiana na jumuiya na mabaraza ya wazee katika ngazi za mkoa, wilaya na shehia ili kusimamia maendeleo ya wazee nchini.

Anasema hadi kufikia Agosti mwaka huu, mabaraza tisa ya wazee yalianzishwa katika ngazi ya wilaya kote Unguja na Pemba hivyo wilaya na shehia zote zimeshakuwa na vyombo hivyo vinavyojadili mafanikio na changamoto mbalimbali zinazowakabili wazee katika maeneo yao.

Waziri Riziki anasema wazee waliopo katika vituo hivyo serikali inaendelea kuwapatia huduma zote za msingi wanazostahiki ikiwamo kuwasimamia, chakula, malazi, mavazi matibabu pamoja na posho.

Rais Dk. Mwinyi pamoja na kuongeza kiwango cha pensheni jamii kwa wazee, ameongeza pia pensheni kwa wastaafu wote kutoka shilingi 90,000 hadi 180,000 kwenye kiwango cha chini.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Sada Mkuya, anasema maamuzi hayo ya kuwa na penshen jamii yanaifanya Zanzibar kuwa pekee katika Afrika Mashariki inayotoa huduma hiyo.

Dk. Sada anasema ongezeko la pensheni kutoka Sh. 2000 hadi 50,000 kulikofanywa na Dk. Mwinyi kunatokana na uchumi na maisha kubadilika, akiona kuna haja ya kuongeza kiwango hicho kwa asilimia 150.

"Wazee wametoa mchango mkubwa kustawisha maisha na serikali, na ndipo Dk. Mwinyi alipotoa ahadi ya kwamba kila hali ya uchumi itakapoimarika na kiwango cha pensheni jamii kitaimarika pia," anasema Waziri Sada.

Aidha anasema wakati pensheni hiyo ilipoanza kutolewa, wazee wakipewa mkononi fedha taslimu lakini kwa sasa wanalipwa kupitia benki na kwamba hatua hiyo ya kulipwa kidijitali inatokana na nchi kwenda na mageuzi ya kiuchumi na kimifumo ya kielektroniki.

Anasema mabadiliko yoyote lazima yatakuja na changamoto na mara ya kwanza kutoa fedha hizo kwa mfumo wa kibenki baadhi ya wazee hawakukubali lakini baada ya kuwapa elimu waliridhia.

## Mtaalamu ataka majumba yahakikiwe kujua uimara, uduni na uhimilivu

INATOKA UK.11

Anadokeza kuwa ni vigumu kulinda viwango na kuwa na ubora na usahihi kama hakuna mshauri anayesimamia kazi hiyo.

Bodi hizo zikishaidhinisha mhandisi msimamizi, anatafutwa na kupewa jukumu la kusimamia na kufuatilia kazi kuona kuwa kila kitu kilichopendekezwa na mkadiria majenzi kinafuatwa na kila siku anakagua na kusimamia badala ya kuacha watu wajifanyie wanavyotaka.

Moshi anasema huenda hiyo ni changamoto hakukuwa na mhandisi mshauri msimamizi kutokana na sababu mbalimbali pengine masuala ya malipo.

Anapoulizwa kuhusu hatua za kufuatilia anasema zinaanza na kuangalia iwapo kazi za ujenzi huo zilisajiliwa na kupewa kibali na kampuni iliyosimamia ujenzi.

Pamoja na kufuatilia hayo, mamlaka pia zifuatilie injinia aliyesimamia na iwapo alifanyakazi kama alivyoelekeza mkadiria majenzi.

Anashauri pia aliyechora ramani naye achunguzwe na kufuatiliwe kikamilifu ili kuondoa changamoto kama hizo siku za usoni.

Anaeleza kuwa majengo yote yaliyojengwa kuanzia miaka ya 2000 ni lazima yamesajiliwa na bodi na mamlaka za miji au majiji.

**MAONI YA WADAU**

Baadhi ya mafundi ujenzi wanaozungumzia skata hilo wanasema baadhi ya wahandisi ujenzi si waaminifu wanaiba vifaa vya ujenzi au kutumia vifaa hafifu ndiyo maana wakati mwingine majanga yanatokea.

"Sementi inaibiwa, nondo na vyuma pia, kokoto, mbao na vingine hupelekwa kwa wahandisi hao ambao wanajenga nyumba zao. Anajenga Tabata, Kinyerezi au mikoani hata Arusha au Mwanza," anasema fundi anayejenga Mikocheni.

Aidha, ofisa mmoja wa DAWASA, Dar es Salaam, anasema ni vyema kuangalia miundombinu ya maji taka ambayo kuna baadhi ya majengo makaro ya maji taka yako chini ya ghorofa.

Anasema maji hayo yanaongeza udhaifu kwenye majengo kwa sababu yanajaa matope na kuwa hatari ghorofa kusimama juu ya matope.

"Kuna uwezekano siku moja baadhi ya majengo yakazama," anasema mhandisi maji jina tunalo.





## 'Tanzania iko vizuri matumizi mfumo jamii namba'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Tume ya TEHAMA nchini (ICTC), Dk. Nkundwe Mwasaga amebainisha kuwa Tanzania ni miongoni mwa mataifa machache duniani ambayo yapo katika hatua nzuri ya matumizi ya mfumo wa jamii namba.

Mfumo huo ni utambulisho wa kipekee unaotolewa kwa kila mwananchi, ambao unatumika katika mifumo mbalimbali ya serikali na sekta binafsi.

Akizungumza jana na Nipashe, mkurugenzi huyo alisema katika kikao kilifanyika miezi miwili iliyopita nchini Misri cha kuangalia nchi gani ambazo zimepiga hatua katika kujiandaa kuweza kutumia hizo namba za namna hiyo, ripoti ilionesha Tanzania ipo katika nchi chache duniani ambazo zimepiga hatua kuwa na mfumo ambao upo tayari.

Dk. Mwasaga alisema kuwa hapa nchini tayari mfumo unaozungumza na kilichobaki sasa ni mifumo kufanya kazi kwa pamoja na wananchi wapewe elimu ianze kutumika.

"Katika kuziwezesha namba hizi kufanya kazi hadi nje ya nchi kuna mfumo wezeshi wa kuwezesha kutumia namba nchi nyingine, sasa hiyo inahitaji nchi za Afrika zikae pamoja, nchi zingine unakuta zimeshakubaliana baina ya nchi na nchi kwenye matumizi ya mfumo wa aina hiyo," alisema.

Alifafanua kuwa Agosti mwaka jana Rais Samia Suluhu Hassan alisisitiza umuhimu wa mfumo huo ili kumaliza utitiri wa utambulisho wa namba zinazotumika sasa na kuwezesha mifumo kusomana nchini.

# TARURA yaonya wanaokata barabara kuchepusha maji

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) Wilaya ya Iramba mkoani Singida umeonya baadhi ya wananchi ambao wamekuwa na tabia ya kukata barabara na kutengeneza mfereji kwa ajili ya kupitisha maji kwenda katika mashamba yao ya mpunga.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Iramba, Evance Kibona, alitoa onyo hilo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara na madaraja katika wilaya hiyo katika kipindi cha kuanzia 2021 hadi 2024.

"Tuna changamoto kwa baadhi ya wananchi hususani maeneo ya mabondeni ambako kuna kilimo cha mpunga mfano Kata ya Mtoa na Gungu wananchi wamekuwa na tabia ya kukata barabara kupitisha maji kuyapeleka kwenye mashamba yao ya mpunga," alisema.

Kibona alisema wananchi lazima watambue kuwa ipo Sheria ya Barabara ya Mwaka 2011 ambayo inaelekeza kutoza faini au kifungo kwa mtu anayefanya uharibifu wa barabara na kwamba TARURA imekuwa ikitoa elimu kupitia kwa viongozi wa vijiji na kata ili kukabiliana na hali hiyo.

Aidha, alisema tatizo lingine ni wananchi kupitisha mifugo kwenye barabara na kufanya uharibifu, kwamba wananchi kujenga majengo kwenye hifadhi ya barabara wakati sheria haziruhusu kufanya hivyo.

Akizungumzia miradi, alisema katika kipindi cha kuanzia mwaka 2022/23 zimejengwa barabara za kiwango cha lami katika Mji wa Kiomboi zenye urefu wa kilometa 2.3 kwa Sh.bilioni 1.6 na katika bajeti ya 2023/24 zimejengwa kilometa 1.5 kwa Sh.bilioni 1.2.

Aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2024/25 zitajengwa barabara zenye urefu wa kilometa 1.6 kwa kiwango cha lami na mwaka jana umeanza ujenzi wa madaraja ya kalavati manne likiwamo lenye ukubwa wa milango 12 urefu wa mita 60 kwa gharama ya Sh.bilioni 2.9.

Alisema daraja hilo lipo Barabara ya Mtoa-Ndago katika Mto Kikunku na ujenzi wake umefikia asilimia 60 na unatarajia kukamilika Januari mwaka 2024/25.

Kibona alisema pia upo ujenzi wa daraja katika barabara mpya iliyofunguliwa ya Masagi-Tyeno ambayo inahudumia wananchi wa kata za Shelui na Mtoa ambalo ina urefu wa mita 20 na litagharimu Sh.milioni 960.

Alisema barabara zote zilizojengwa kwa kiwango cha lami, zimewekewa taa hali ambayo imeongeza uchumi kwa wananchi kwa sababu wanafanya shughuli zao za ujasiriamali muda wote sasa.

Alisema: "Tunaishukuru sana serikali kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja sasa hivi barabara nyingi zimefunguka na zinapitika muda wote katika wilaya yetu ya Iramba."




Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, akifungua mafunzo kwa wahasibu wanawake kutoka halmashauri zote za Tanzania Bara ili kuwajengea uwezo wa usimamizi wa fedha za umma, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC ahimiza wanawake kuchangamkia mikopo ya halmashauri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewafunda wanawake kuchangamkia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri mbalimbali, badala ya kukimbilia mikopo ya 'kausha damu'.

Senyamule alitoa wito huo mwishoni mwa wiki kwenye Kongamano la Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi mkoani hapa.

Alisema serikali isingependa kusikia malalamiko ya wanawake kupokonywa vitu kutokana na kuchukua mikopo umiza mitaani, wanachotakiwa ni kutumia fursa za mikopo inayotolewa na serikali kwa riba nafuu ili kujiinua kiuchumi.

Alibainisha kuwa serikali imeshatoa maelekezo kwa halmashauri kuhusu utoaji wa mikopo hiyo kwa wanawake na taratibu za utoaji zinakamilishwa.

Kutokana na hilo, aliwataka wanawake walioko kwenye vikundi na ambao hawana vikundi waungane kwa ajili ya kupata elimu ya nini wanatakiwa kufanya ili wapate mikopo hiyo kwa ajili ya kuendesha biashara zao.

"Nisingependa kuona malalamiko ya kunyang'anywa vitu vya ndani kutokana na kushindwa kulipa mikopo umiza mnayochukua kwa watu binafsi, tumieni fursa ya mikopo inayotolewa na serikali," alisema Senyamule.

Kadhalika alisema kuna baadhi ya wanawake wanatumia fursa za mikopo ya serikali na kuondokana na adha ya mikopo hiyo.

Naye Ofisa Maendeleo wa Mkoa wa Dodoma, Happy Hiza, alisema wao kama sehemu ya wahusika wa mikopo hiyo, hawawezi kumfuata mtu mmoja mmoja kila kaya.

Alisema bali wanawake wanatakiwa kuunda vikundi vyao wakiwa na vigezo husika kwa ajili ya kupata mikopo hiyo.

"Wanawake tumieni fursa ya hii ya mikopo ili mjikwamue kiuchumi, msikae kulalamika pembeni, mnachotakiwa ni kufika katika ofisi za halmashauri kupata maelekezo juu ya mikopo hiyo," alisema Hiza.

Alisema serikali imeshatoa maelekezo kuhusu utoaji mikopo hiyo, kinachotakiwa kwa wajasiriamali ni kufuatilia taratibu zinazotakiwa ili kupata mikopo ambayo itawasaidia kupanua wigo wa ujasiriamali wanaofanya.

Mwenyekiti wa jukwaa hilo mkoani hapa, Maryrhobi Mabhaya, aliishukuru serikali kutokana na kurejesha mikopo pamoja na fursa nyingine ambazo zinawasaidia wanawake kujikwamua kiuchumi.

Mabhaya alisema wamekuwa wakitoa elimu ya namna ya upatikanaji mikopo kupitia wataalamu kutoka taasisi mbalimbali za fedha, ili kuwapa mwongozo wa kutanua wigo wa ujasiriamali wanaoufanya na kujikwamua kiuchumi.

Alisema suala hilo limeonyesha mwamko mkubwa kwa wanawake wajasiriamali kufikiria kufanya biashara kubwa zenye lengo la kupiga hatua kimaendeleo.



# Wasiojulikana waiba dira, mifuniko ya majitaka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wasiojulikana wameiba zaidi ya dira 2,000 za maji na mifuniko 50 ya mashimo ya majitaka kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya.

Hali hiyo imesababisha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) hasara ya zaidi ya Sh. milioni 170.

Aidha, baadhi ya wananchi wa Jiji hilo wasiokuwa waaminifu wanadaiwa kuhujumu miundombinu ya maji kwa kujiunganishia huduma hiyo hali ambayo inadaiwa kuwa chanzo cha kuharibu ubora wa huduma kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu tathmini ya hali ya hujuma ya miundombinu ya maji na hali ya upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Alisema wimbi la wizi wa vifaa hivyo limeshamiri na kwamba mpaka sasa hawajabaini kazi ambayo wanakwenda kufanyia watu wanaoiba vifaa hivyo.

Alisema kutokana na tatizo hilo mamlaka hiyo kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama imeanza kufanya operesheni ya kuwasaka wahalifu hao na kuwachukulia hatua za kisheria.

"Mpaka sasa tumeshawakamata watu 12 wakihusishwa na hujuma hizi na wengine tayari tumeshawafikisha mahakamani na kuwafungulia kesi ya uhujumu uchumi, kwa hiyo tutaendelea kuchukua hatua dhidi ya wote watakaobainika," alisema Kayange.

Alisema dira moja ya maji inanunuliwa na mamlaka hiyo kwa Sh. 80,000 na mfuniko mmoja wa mashimo ya majitaka unauzwa Sh. 200,000 na kwamba dira hutolewa bure kwa wananchi wanapounganishiwa huduma ya maji kwa mara ya kwanza.

Hivyo, aliwataka wananchi wa maeneo mbalimbali kushiriki kulinda miundombinu ya maji kwa kuhakikisha wanatoa taarifa za wale wanaohujumu miundombinu, ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Alisema kwa mwananchi yeyote ambaye atatoa taarifa ambazo zitafanikisha kukamatwa kwa watu wanaohujumu miundombinu hiyo atapata zawadi ya Sh. 1,000,000.

Pia, aliwataka watu wanaofanya vitendo hivyo kuacha mara moja kwa maelezo kuwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi, huku akidai watakaotoa taarifa zitabaki kuwa siri ya ofisi.

Alisema menejimenti ya mamlaka hiyo inaendelea kufanya ufuatiliaji wa mtaa kwa mtaa katika maeneo yote ya jiji hilo ili kusikiliza kero za wananchi, kuzitatua pamoja na kufanya tathmini ya wizi wa miundombinu.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), Gilbert Kayange, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki (hawapo pichani), alipotoa taarifa ya hujuma za miundombinu ya maji zinazofanywa na watu wasiokuwa waaminifu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waomba ukarabati wa barabara wasafirishe mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Ilungu wilayani Mbeya wameiomba serikali kuzifanyia marekebisho barabara wanazotumia kusafirisha mazao kutoka shambani kabla ya msimu wa mvua kuanza.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi hao walisema kuwa serikali kupitia kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) imekuwa na kawaida ya kukarabati barabara wakati wa mvua jambo ambalo huwakwamisha kutoa mazao shambani na kuathiri uchumi wao.

Mkazi wa Kijiji cha Ifupa, Leonard Mwayonga alisema kuwa msimu wa mvua za vuli katika kata yao huanza Desemba ambapo na wao huanza shughuli za kilimo.

Alisema serikali inapoanza kukarabati barabara Februari wakati huo mvua huwa zinanyesha huku mazao yao nayo huwa yamekaribia kukomaa na kuhitaji kuvunwa.

Kwa upande wake Motema Kyando ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Masesye alisema zao kuu wanalolima kwenye kata hiyo ni viazi mviringo ambavyo vinapovunwa ni lazima visafirishwe kwa wakati kwenda sokoni kwa sababu vikichelewa huharibika.

Akizungumzia kero hiyo ya wananchi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema anatambua kuwa Kata ya Ilungu ni wakulima wazuri na kwamba matatizo yao ameyapokea.

Alisema anatarajia hivi karibuni kufanya ziara kwenye kata hiyo kwa lengo la kwenda kuzungumza na wananchi na kusikiliza kero zao ili azitafutie ufumbuzi.

Alisema wakati wa ziara hiyo ataongozana na wataalamu mbalimbali wakiwamo maofisa wa TARURA, hivyo anaamini kero ya barabara kwa wananchi hao itapata majibu.

# Polisi: Msiwatumie 'vishoka' kupata leseni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewataka madereva wanaotaka kupata leseni ama kuhuisha leseni zao kuacha kuwatumia 'vishoka' na badala yake wafuate taratibu za kisheria ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha wadau wa usafirishaji kilichokuwa na lengo la kutatua kero mbalimbali za usafirishaji.

Alisema baadhi ya madereva wamekuwa wakiwatumia vishoka kupata leseni ama kwenda kuhuisha leseni zao hali ambayo inasababisha kutokamilika kwa baadhi ya michakato na kwamba wakati mwingine wanapata leseni watu wasiokuwa na sifa.

Alisema dereva yeyote anayetaka kupata leseni anatakiwa kupeleka nyaraka zake katika Ofisi ya Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa ili zikaguliwe na kumfanyia majaribio dereva huyo kabla ya kupatiwa leseni.

Alisema baada ya kujiridhisha RTO anaandika mapendekezo yake kwenda kwa RPC kwa ajili ya kumteulia daraja la kupatiwa kwenye leseni, huku akisisitiza kwamba mhusika ndiye anakwenda kwa RPC ili kujiridhisha.

"Ukimtuma kishoka hawezi kuingia kwangu kwa sababu nitataka kujiridhisha kwa kumwangalia yeye na kumfananisha na picha iliyopo kwenye vyeti vyake, kwa hiyo akija kishoka lazima tutamuweka ndani," alisema Kamanda Kuzaga.

Awali mmoja wa madereva walioshiriki kwenye kikao hicho, David Jackson alisema madereva wamekuwa wakikumbana na urasimu wakati wa kufuatilia leseni zao katika ofisi za Jeshi la Polisi hali ambayo wakati mwingine huwa inasababisha waanze kufikiria njia za mkato.

Alisema huwa wanazungushwa bila sababu na hivyo kama mtu ni mgeni akikutana na kishoka inakuwa rahisi kumwamini na hivyo kuamua kumtumia badala ya kufuata taratibu zilizoko.

Hivyo, aliliomba Jeshi la Polisi kuwasaidia kuondoa urasimu huo ili kuwarahisishia madereva kupata nyaraka hiyo muhimu inayowapatia uhalali wa kuendesha magari.

Kikao hicho kiliwashirikisha maofisa wa Jeshi la Polisi, madereva, maofisa wa Mamlaka ya Udibiti wa Usafiri wa Majini na Ardhini (LATRA) pamoja na wadau wengine wa usafirishaji.





## RC ahimiza wananchi kutumia fursa kujikwamua kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, amewataka wananchi wa mkoa huo kuzitumia fursa zinazotolewa na serikali katika kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Alisema miongoni mwa fursa hizo ni Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia ambayo ina manufaa makubwa katika kuimarisha uchumi wa wananchi wenye kipato duni.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa programu hiyo ambayo imezinduliwa kwa mara ya kwanza visiwani Zanzibar ambayo inawashirikisha wajasiriamali wa Zanzibar wakiwamo wa Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kwa muda mrefu wananchi wakipata uwezeshaji kwa miundombinu mbalimbali ikiwamo ujenzi wa barabara, afya, maji na miundombinu mingine lakini dhamira ya Dk. Samia na Dk. Mwinyi ni kuwanufaisha wananchi wenye kipato cha chini kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Aidha, alisema wakazi wa Kusini wana faraja kubwa kupewa heshima hiyo kwa sababu programu hiyo ni dhamira njema ya Rais Dk. Samia kuwawezesha kiuchumi.

Ayoub alisema kuwa mchakato wa kuwezeshwa kupitia programu hiyo ni muhimu, hivyo aliwataka wananchi wa mkoa huo wasichezee fursa hiyo bali ni kuitunza na kuidumisha.

Alisema kwa mkoa huo programu hiyo itahusisha watu 700, watakwenda kupunguza changamoto ya maisha kwa watu zaidi ya 30,000 kwa Zanzibar na hiyo ni dhamira njema ya Rais kwa wananchi wake.

Hivyo, alitumia fursa hiyo kuwataka kuwa mabalozi katika maeneo yao ili wananchi wote wenye kipato cha chini waweze kuwezeshwa kupitia programu hiyo.

Pia, aliipongeza IMASA kwa kuandaa jambo hilo ambalo lina manufaa makubwa kwa wananchi wa Tanzania wenye kipato cha chini kwa ajili ya kusaidia wananchi kiuchumi na kuondoa umaskini.

Naye Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, akitambulisha programu hiyo imelenga kuwainua wananchi kiuchumi kwa kuwatoa walipo na kwenda mbele zaidi kimaendeleo.

Alisema programu hiyo pia imelenga kuwanufaisha makundi ya wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu hivyo wananchi wanaofanya shughli zao za kujikwamua kiuchumi lazima kufanya kwa weledi.

Alisema kwa Zanzibar ili kunufaika na programu hiyo ni lazima kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Zanzibar (ZEA).

Naye Mkurugenzi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA), Juma Burhan alisema ZEA inajukumu la kuwawezesha wananchi katika idara ya mikopo na uwezeshaji, mafunzo na masoko na idara ya viwanda.

# Wananchi walia makali ya bei gesi ya kupikia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wa Kisiwa cha Uzi Ng'ambwa Mkoa wa Kusini Unguja wameitaka serikali kupunguza gharama ya nishati safi ya kupikia, ili kuwapa unafuu wa kutumia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Wakizungumza na Nipashe kisiwani humo, walisema licha ya serikali kupitia Rais Samia Sukuhu Hassan kuletewa nishati ya gesi ya kupikia lakini kutokana na hali ngumu ya kiuchumi waliyokuwa nayo wanashindwa gharama za kuendeleza matumizi ya nishati hiyo.

Asha Ramadhan Bakari, alisema bei ya gesi ni kubwa ambapo mtungi wa kilo tano wananunua kwa shilingi 25,000 jambo ambalo ni gharama kubwa kwao wakati nishati ya kuni wanaipata bila ya gharama yoyote.

"Kwa kweli tunamshukuru Rais Mama Samia kwa kutuletea nishati ya gesi ya kupikia, tunatumia maana tumeletewa tuachane kuharibu mazingira, lakini tunaombi kwake tupunguziwe bei ya gesi maana ndiyo sababu inayotupelekea kuendelea kutumia kuni na mkaa," alisema.

Salama Mwijangao Abdallah mkazi wa kisiwa hicho, alisema yeye ni miongoni mwa wanufaika wa gesi asilia iliyotolewa na Rais Samia ambapo matumizi ya nishati hiyo imeongeza mapenzi na mahaba kutoka kwa mume wake kwa sababu chakula kukiandaa mapema.

Alisema licha ya kunufaika lakini bado gharama za matumizi ya nishati hiyo zipo juu, hivyo alitaka serikali na kampuni ya gesi kupunguza gharama za nishati hiyo ili wananchi wanyonge nao kumudu gharama za nishati hiyo.

Humud Talib Ali mkazi wa kisiwa hicho, alisema hali ya mazingira katika kisiwa hicho imebadilika ikilinganishwa na zamani kwa sababu hata upatikanaji wa samaki baharini umepungua.

Akizungumzia kuhusu matumizi ya nishati ya gesi asilia, alisema gharama ya nishati hiyo ipo juu na hali za kiuchumi kwa wananchi wa kisiwa hicho ni ngumu.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA, Zanzibar) Dk. Mzuri Issa, alisema chama hicho kwa kushirikiana na wadau wao ambao ni Shirika la Kimataifa la Misitu, Jumuiya ya Misitu Pemba kupitia ufadhili wa Serikali ya Canada wanatekeleza mradi wa ZANADAPT.

Alisema mradi huo unaohusiana na mazingira ambao unalenga kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi kwa kutoa elimu kwa wananchi hasa wanawake katika kuhifadhi mazingira na kukabiliana na athari hizo.

Alisema bado habari za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hazijaandikwa kwa wingi ikilinganishwa na habari zingine, hivyo kupitia mradi huo pia inatoa elimu kwa waandishi wa habari ili kufanya uchechemuzi katika kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi.

Alisema matumizi ya gesi salama itasaidia kulinda na kuhifadhi mazingira, hivyo ni vyema wanawake kuwezeshwa kiuchumi ili kumudu gharama za nishati hiyo kwa ajili ya kupikia.



Mkazi wa Kisiwa cha Uzi Zanzibar, Asha Ramadhan Bakari, akiandaa kuni zake kwa ajili ya kupikia, hali ambayo inachangia uharibifu wa mazingira. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waandishi IPP wapewa vyeti mchango katika takwimu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

OFISI ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar imetoa vyeti vya shukrani kwa waandishi wa habari, asasi za kiraia na vyombo vya habari kutokana na mchango wao katika kuelimisha jamii kuhusu masuala ya takwimu.

Miongoni mwa vyombo vya habari vilivyopewa vyeti hivyo ni waandishi wa habari wa kampuni ya IPP Media visiwani Zanzibar.

Waandishi wa habari wa IPP Media waliotunukiwa vyeti hivyo ni mwandishi wa wa Nipashe, Rahma Suleiman pamoja na Farouk Karimu wa ITV visiwani humo.

Akizungumza baada ya hafla hiyo iliyokwenda sambamba na Siku ya Takwimu Afrika ambayo huadhimishwa Novemba 18 ya kila mwaka, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema waandishi wa habari wanamchango mkubwa katika kutoa taarifa kwa jamii hasa zinazohusiana na takwimu.

Alisema kutokana na kauli mbiu ya Siku ya Takwimu isemayo 'Kuwezesha utoaji wa elimu kwa takwimu kwa madhumuni ya kufikia maendeleo' ambapo vyombo vya habari vinamchango mkubwa wa kutoa elimu za takwimu na kuelimisha jamii.

"Kwa dhati kabisa navipongeza vyombo vya habari, asasi za kiraia, wananchi na wadau wote kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika kukusanya na kuchambua na kuzitoa takwimu mbalimbali zinazozalishwa na ofisi ya mtakwimu," alisema.

Alisema waandishi wa habari pamoja na vyombo vya habari ni mstari wa mbele katika kutoa elimu na uelewa kuhusu umuhimu wa takwimu na elimu hizo ni chachu ya uzalishaji wa takwimu zinazozalishwa.

Alisema waandishi wa habari wanajukumu kubwa la kutoa habari na kuelimisha jamii na sekta ya habari imelifanyia kazi hilo na ndio maana wameamua kutoa vyeti vya shukrani kwao.

Aidha, alisema waandishi wa habari ni daraja kubwa lenye thamani katika kusambaza na kutangaza takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kila mwezi kama ilivyopewa jukumu ya kuzalisha takwimu za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mery Khatib, aliwataka waandishi wa habari kuendelea kutoa elimu na taarifa za takwimu kusikika na kuelimisha jamii, kusiadia elimu kwa njia ya kisasa ya uzalishaji wa takwimu zinazofaa.

Aidha, alisema kwa kutumia ukusanyaji wa data kwa hali ya juu na mbinu za uchambuzi, taasisi ya elimu na watunga sera wameweza kupata taarifa sahihi na kwa wakati ambapo zitaakisi mahitaji na changamoto zilizopo katika sekta ya elimu.

Alisema juhudi hizo zinalenga kulingana na matukio mahasusi ya elimu, kuwezesha utambuzi wa upungufu katika ufikiaji, ubora na usawa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**NAMAYANI RAPEY EDWARD** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE 043473.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/44255/2024.**

## KUBADILISHA JINA




Mwenye picha hapo juu anatangaza kubadilisha jina lake lililokosewa ambalo ni **SAIDI MRADI NANCHINGA.** Jina lake sahihi ni **SAIDI MRADI ATHUMANI** kwa mujibu wa sheria.

## KUPOTEA KWA CHETI



**OSCAR MICHAEL JOVIT** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4818-0256** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **GWEGENYEZA SEC SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/252831/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TAJIRI SANNE LOOSINIGI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S5725/0083** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MATALE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2022, Cheti hiki kimepotea Jijini DODOMA. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/51932/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KAWEDI MAKITURU MONGI,** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 507 BYX** aina ya **TOYOTA MARK II,** Chassis No. **SX900001234,** Engine No **4SFE4328.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. **9910843083452**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALBINA VICENT BIZURU**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.158 DDN** aina ya Toyota **NOAH,** Mali ya **ROYAL SUPER MARKET** yenye Chassis No. **RCH410020381,** Engine No.**3RZ1679909** yenye rangu nyeupe. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi; **PHQ/SHI/KAH/11249/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MSUSA KHALIFA HOKORORO**

anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba **MC 901 DVK.** CHASIS NO: **MD2B15BX2PWM89712.** ENGINE NO: **JVXWPM56850. MC 902 DVK.** CHASSIS NO: **MD2B15BX4PWM89713.** ENGINE NO: **JVXWPM56797. MC 906 DVK.** CHASSIS NO: **MD2B15BX1PWM89717.** ENGINE NO: **JVXWPM56823.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi: Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/KYE/4808/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No....../ 2024**

**In the matter of the Estate of the late LAWRENCE MBOGO PYUZA of Iyumbu Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY LUSIA LAWRENCE PYUZA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 22 Day of 11, 2024
Date at Dodoma this 10TH Day of OCTOBER, 2024.

.................................
PETITIONER

Presented for filing this.................................day of..............................2024

.................................
RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA KIHONDA** **MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...48/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEMU: HENRY AUGUSTINO SELEMANI wa MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MWANAHAWA ALLY ISMAIL**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 18 mwezi 11 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA
MOROGORO

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 344 LA 2024**

**SALIM MBAROUK MUOMBAJI/ WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **MARIA B. MOMBA**
2. **ARON EVAREST.....................MDAIWA / WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **MARIA B. MOMBA**
2. **ARON EVAREST**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**SALIM MBAROUK** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni(Mwananyama) Shauri husika limepangwa kutajwa / kusikilizwa tarehe 12/12/2024 saa 03:00 Asubuhi mbele ya **Mh. J.W. SILLAS** Hivyo unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 13 Mwezi 11 Mwaka 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie: +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Marekani yairuhusu Ukraine kutumia makombora makubwa

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden ametoa ruhusa kwa Ukraine kutumia makombora ya masafa marefu yaliyotolewa na Marekani kuishambulia Russia ambayo iko kwenye mzozo wa vita kwa muda mrefu.

Hayo yalibainishwa na ofisa wa Marekani aliyezungumza kwa sharti la kutotajwa jina, na hivyo kuthibitisha taarifa zilizochapishwa na vyombo vya habari vya taifa hilo na ambayo inaashiria mabadiliko makubwa ya sera ya Marekani, juu ya vita hivyo.

Kwa miezi kadhaa, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alikuwa akitaka vikwazo dhidi ya makombora hayo yanayojulikana kama ATACMS viondolewe ili kuiruhusu Kyiv kufanya mashambulizi nje ya mipaka yake.

Akijibu ruhusa hiyo kiongozi huyo alisema mambo kama hayo hayatangazwi, makombora yanajieleza yenyewe.

Rais wa Russia, Vladimir Putin, siku chache zilizopita aliyaonya mataifa ya Magharibi dhidi ya hatua hiyo, akisema itamaanisha kuwa muungano wa kijeshi wa Nato unashiriki moja kwa moja katika vita vya Ukraine.

Ilielezwa kuwa bado Putin hajatoa maoni yake kuhusu ripoti hiyo, lakini wanasiasa wengine wakuu wa Kremlin wameelezea hatua hiyo kama ya kukuza vita. Uamuzi wa Washington juu ya ATACMS unahusiana tu na kushambulia mkoa wa Kursk wa Russia, ambako Kyiv ilifanya uvamizi wa kushtukiza mwezi Agosti.

Utawala wa Rais Biden unaiambia Ukraine, kwamba inaunga mkono juhudi zake za kuishikilia sehemu ndogo ya eneo la Russia ambayo inaikalia hivi sasa, kama mtaji wa mazungumzo yoyote yanayoweza kutokea katika siku zijazo.

Serhiy Kuzan, mwenyekiti wa Kituo cha Usalama na Ushirikiano cha Ukraine chenye makao yake makuu mjini Kyiv, aliambia BBC kuwa, uamuzi wa Rais Biden ni muhimu sana kwa nchi hiyo.

"Sio jambo litakalobadilisha mkondo wa vita, lakini nadhani litafanya vikosi vyetu kuwa imara," alisema.

Makombora ya ATACMS yanaweza kufika hadi kilomita 300 (maili 186). Maofisa wa Marekani ambao hawakutajwa majina wameyaambia magazeti ya New York Times na Washington Post kwamba Biden kutoa ruhusa kwa Ukraine kutumia silaha hizo kumekuja baada ya uamuzi wa Russia kuruhusu wanajeshi wa Korea Kaskazini kupigana nchini Ukraine.

Kuzan alisema uamuzi huo umekuja kabla ya shambulio lililofanywa na wanajeshi wa Russia na Korea, ili kuviondoa vikosi vya Ukraine kutoka eneo la Kursk nchini Russia.

Ukraine inakadiria kuwa kuna wanajeshi 11,000 wa Korea Kaskazini huko Kursk, na kwamba uamuzi wa Rais Biden pia utaziwezesha Uingereza na Ufaransa kuipa Ukraine idhini ya kutumia makombora ya masafa marefu ya Storm Shadow ndani ya Russia. **BBC**



Rais wa Marekani, Joe Biden (kulia), akisalimiana na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky. **PICHA: MTANDAO**

# Wagabon wapitisha rasimu katiba mpya

**LIBREVILLE,** Gabon

SERIKALI ya nchini Gabon imesema wapigakura nchini humo wameidhinisha kwa wingi katiba mpya, ikiwa ni zaidi ya mwaka mmoja baada ya wanajeshi walioasi kumpindua rais wa muda mrefu wa nchi hiyo na kuchukua mamlaka.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Gabon, Hermann Immongault, alisema katika taarifa yake iliyosomwa kwenye televisheni ya taifa kwamba zaidi ya asilimia 91 ya wapigakura wameidhinisha katiba mpya katika kura ya maoni iliyofanyika Jumamosi.

Kiongozi huyo alisema waliojitokeza walikadiriwa kuwa asilimia 53.5 na kwamba matokeo ya mwisho yatatangazwa na Mahakama ya Katiba.

Ilielezwa kuwa rasimu ya katiba, ambayo inapendekeza mabadiliko makubwa ya kimamlaka ilihitaji zaidi ya asilimia 50 ya kura zilizopigwa ili kupitishwa. **VOA**

## 96 wauawa na Israel Gaza

**GAZA,** Palestina

MAMLAKA za mitaa katika Ukanda wa Gaza zimesema kuwa takriban Wapalestina 96 wameuawa na wengine 60 kujeruhiwa katika mashambulizi ya anga ya Israel yaliyofanyika kaskazini mwa ukanda huo.

Kwa mijibu wa taarifa za mamlaka hizo, mashambulizi hayo yalifanyika jana na kwamba jeshi la uvamizi lilifahamu kwamba makumi ya raia waliokimbia makazi yao walikuwa ndani ya majengo hayo yaliyoshambuliwa.

Ilielezwa kuwa waliodhurika wengi wao walikuwa watoto na wanawake ambao walikuwa wamehamishwa kutoka kwa vitongoji vyao, huku mamlaka hizo zikiitaka jumuiya ya kimataifa kukemea.

"Tunaomba jumuiya za kimataifa kukemea mauaji haya ya kutisha dhidi ya raia waliokimbia makazi yao na kutaka uwajibikaji kwa serikali ya Israel na waungaji mkono wake wa kimataifa, ikiwa ni pamoja na Marekani, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa," ilisema sehemu ya taarifa ya mamlaka.

Aidha, huko Lebanon ilielezwa kuwa Israel iliripoti kurushwa kwa roketi kutoka Lebanon na ndege isiyo na rubani kutoka Iraq huku mvutano wa kikanda ukiendelea kuongezeka kutokana na vita vinavyoendelea vya Tel Aviv dhidi ya Gaza.

Channel 7 ya Israel ilisema kuwa roketi 15 zilirushwa kutoka Lebanon kuelekea Acre na Haifa Bay kaskazini mwa Israel.

Jeshi la Israel pia lilisema kuwa vikosi vyake viliikamata ndege isiyo na rubani iliyorushwa kutoka mashariki, neno linalotumiwa na jeshi kuelezea mashambulizi kutoka Iraq.

Pia ilielezwa kuwa idadi ya vifo kutokana na mashambulizi ya Israel huko Gaza yameongezeka hadi 43,846.

Takriban Wapalestina 43,846 waliuawa na 103,740 kujeruhiwa katika mashambulizi ya kijeshi ya Israel huko Gaza tangu yalipoanza Oktoba 7, 2023, wizara ya afya ya Gaza ilisema.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Waisraeli watatu walikamatwa kwa shambulio la bomu kwenye nyumba ya Netanyahu kaskazini mwa Israel

Ilielezwa kuwa Polisi wa Israel waliwakamata watu watatu kufuatia kurusha mabomu katika nyumba ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu kaskazini mwa Israel.

Gazeti la kila siku la Israel Yedioth Ahronoth lilisema mmoja wa washukiwa waliokamatwa ni ofisa mkuu wa akiba, Brigedia jenerali, ambaye amekuwa akifanya maandamano dhidi ya serikali ya Netanyahu katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. **TRT**

# HAMZA: NITAREJEA HIVI KARIBUNI UWANJANI

Na Faustine Feliciane

BAADA ya kuwa nje kwa zaidi ya wiki tatu, beki wa kati wa klabu ya Simba, Abdulrazaq Hamza, amesema kwa sasa anaendelea vizuri na anajiandaa kurejea uwanjani.

Beki huyo ambaye yupo nje akiuguza jeraha la mguu baada ya kuumia, amesema akirejea uwanjani ana deni kwa mashabiki wa klabu hiyo.

**"Kwa sasa naendelea vizuri, napambana kuhakikisha narejea haraka uwanjani kuendelea kupigania timu yangu," alisema Hamza.**

Aidha, amesema anawashukuru mashabiki wa timu hiyo kwa namna wanavyoonyesha kiu ya kumuona tena uwanjani akiitumikia klabu yao.

"Nawashukuru sana mashabiki, wamekuwa wakiniombea nirejee haraka uwanjani, wameonyesha mapenzi makubwa, nina deni kwao nitakaporejea uwanjani," alisema.

Hamza, alisema atahakikisha anapambana kuisaidia timu yake kufikia malengo yao msimu huu na kuwalipa fadhira mashabiki wa timu hiyo ambao wamekuwa upande wao.

Mbali na Hamza, pia kiungo mkabaji wa timu hiyo, Yusuph Kagoma, naye yupo nje akiuguza jeraha la mguu baada ya kuumia kwenye mchezo wa dabi dhidi ya Yanga Oktoba 19.



Baadhi ya watoto wanaolelewa kituo cha Sinza Maalum wakifuatilia hotuba ya Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Dar es Salaam, Aidan Komba (hayupo pichani), kabla ya kupokea misaada mbalimbali. NA MPIGAPICHA WETU

## Biashara United yaing'ang'ania kooni Mtibwa Championship

Na Adam Fungamwango

TIMU ya Mtibwa Sugar imeshindwa kupanda pointi tatu katika harakati zake za kutaka kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Biashara United katika mchezo mkali wa ligi ya Championship uliochezwa juzi, Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Wenyeji ndiyo walioanza kutangulia kwa bao la mapema tu lililowekwa kwenye kamba na January Benson, kabla ya straika hatari, Raizin Hafidh kuisawazishia Mtibwa dakika moja kabla ya kwenda mapumziko.

Bao hilo linakuwa la nane kwenye ligi hiyo kwa mchezaji huyo wa zamani wa Coastal Union, Gwambina na Dodoma Jiji.

Straika wa zamani wa Yanga, Ditram Nchimbi aliifungia Biashara United iliyoshuka daraja msimu wa 2021/22, lakini dakika mbili kabla ya mechi kumalizika, Erick Kyaruzi, aliisawazishia Mtibwa.

Sare hiyo inaifanya Mtibwa Sugar kuwa kuleleni mwa msimamo wa Ligi hiyo lakini kwa sasa ikiizidi mabao Geita Gold, huku zote zikiwa na pointi 20.

Mtibwa na Geita Gold ambazo zote zilishuka daraja msimu uliopita zimecheza michezo tisa, zikishinda sita, sare mbili na kupoteza moja kila moja, lakini wakata miwa wana mabao 15 ya kufunga, huku wachimba madini wakiwa na mabao 11.

## Watoa misaada watoto Sinza Maalum

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya kufanikisha kwa mbio za Tigo Marathon 2024 zilizofanyika Zanzibar Novemba 3, kampuni hiyo mwishoni mwa wiki imetoa misaada mbalimbali kwenye kituo cha Sinza Maalum jijini Dar es Salaam chenye watoto zaidi ya 90.

Misaada hiyo imetolewa ikiwa ni sehemu ya kampuni hiyo kurejesha faida kwa jamii.

Akizungumiza baada ya kutoa msaada huo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa kampuni hiyo kanda ya Dar es Salaam, Aidan Komba, alisema kuwa wanatambua umuhimu wa watu wenye mahitaji maalumu na kuona ulazima wa kurejesha kwa jamii faida wanayoipata.

Misaada iliyotolewa kituoni hapo mbali na vitu vingine, ni pamoja na charahani, magodoro, chupa na mahotipoti kwa ajili ya kuhudumia jamii hiyo yenye uhitaji maalumu.

Kwa upande wake, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Catherine Msese aliishukuru kampuni hiyo kwa msaada walioutoa kwa ajili ya shule hiyo.

"Kwa kweli msaada huu utawasaidia watoto kujimudu katika kufanya kazi zao za kila siku kwani tumepata vifaa vya usafi, vitawasaidia watoto katika kufanya usafi hapa shuleni na vifaa vya cherehani vitawasaidia katika mafunzo ya ufundi, lakini pia michezo," alisema Msese.

Kampuni hiyo katika kuendeleza kurudisha kwa jamii, imepanga kuendelea kutoa misaada hiyo kwa kanda zote tisa nchini ambapo mwishoni mwa wiki wameanza na kanda ya Dar es Salaam.

## Malindi SC haishikiki Ligi Kuu Zanzibar

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

USHINDI wa mabao 2-0 walioupata juzi kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Zanzibar dhidi ya Mwenge FC umetosha kuipandisha Malindi SC mpaka nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Matokeo hayo yameifanya Malindi kufikisha pointi 22 na kuapnda nafasi moja mpaka nafasi ya tatu huku wapinzani wao, Mwenge FC wakisalia nafasi ya 14 wakiwa na pointi 10.

Katika mchezo huo wa juzi uliochezwa Uwanja wa Mau A, Malindi SC walionekana kupania ushindi kutokana na kucheza soka la kasi muda wote.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Mohamed alisema mpago wao ni kuhakikisha wanakaa kileleni katika msimamo wa ligi mpaka mzunguko wa kwanza unakamilika.

Alisema mpango huo utafanikiwa kwasababu ya hamasa kubwa waliyokuwa nayo wachezaji wao hasa katika kuhakikisha wanaendelea kupata matokeo mazuri.

Alisema katika michezo yao minne iliyobaki ya kukamilisha mzunguko huu wa kwanza wamejipanga kuhakikisha wanapambana na hawapotezi mchezo.

"Timu inapata matokeo mazuri kwa hili tunashukuru ingawa ipo michezo ambayo tumepoteza lakini haikuwa mingi, hivyo tunaendea na maandalizi ya kuhakikisha michezo yetu iliyobaki tunashinda yote," alisema Mohamed.

Aidha, akizungumzia mchezo dhidi ya Mwenge FC, alisema mchezo huo ulikuwa mgumu kutokana na wapinzani wao kupania kupata ushindi.

Alisema ingawa alipata bao la kwanza katika dakika la mapema lakini wapinzani wao walicheza kwa matumani katika kipindi chote cha mchezo lakini bahati ilikuwa kwao zaidi na kufanikiwa kupata ushindi huo.

ZISIKUPITE

## GYOKERES NA MAN UNITED

MANCHESTER United wameambiwa kuwa Sporting huenda wakamuuza mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres, 26, lakini sio katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Mirror)***

## ...QUENDA PIA ATAKIWA

KLABU ya Manchester United pia inajaribu kutaka kumnunua winga wa Sporting mwenye umri wa miaka 17, Geovany Quenda raia wa Ureno. ***(A Bola)***

## SZCZESNY MKATABA MPYA

BARCELONA inafikiria kumpa kipa Wojciech Szczesny, 34, mkataba mpya wiki chache baada ya raia huyo wa Poland kujiunga na klabu hiyo. ***(Marca)***

## CARLOS KUUZWA JANUARI

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery anaweza kuamua kumuuza mlinzi wa Brazil, Diego Carlos, 31, Januari. ***(Football Insider)***

## NEYMAR KUREJEA SANTOS

WINGA wa Brazil Neymar, 32, anatazamiwa kurejea Santos huku klabu yake ya Saudi Arabia, Al-Hilal ikifadhaishwa na matatizo ya majeraha ya mara kwa mara. ***(Cesar Luis Merlo)***

## KOKCU AMSIFIA ORKUN SLOT

KIUNGO wa kati wa Benfica na Uturuki, Orkun Kokcu, 23, amesifu mchango ambao kocha wa Liverpool, Arne Slot amekuwa nao kwenye maisha yake ya soka huku kukiwa na uwezekano wa kuhamia Anfield. ***(Liverpool Echo)***

## IGOR JESUS ATAKIWA FULHAM

KLABU ya Fulham imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Igor Jesus, 23, kutoka Botafogo. ***(TBR Football)***

## SPURS YAMTAKA TENA WINKS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaangalia uwezekano wa kumsajili tena kiungo wa kati wa England, Harry Winks, 28, baada ya kumuuza kwa Leicester City mwaka jana. ***(Fichajes)***

## YAMGANDA VLAHOVIC

ARSENAL bado inafuatilia hali ya mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic, 24, katika klabu ya Juventus. ***(Rudy Galetti)***


## YATAKA MSHAMBULIAJI

KLABU ya Crystal Palace ina nia ya kusajili mshambuliaji wakati kwenye uhamisho wa Januari lakini wana bajeti ndogo tu. ***(NipeSport)***

## KVARATSKHELIA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, 23, anaweza kuondoka Napoli kwa vile mazungumzo yake ya mkataba mpya yamekwama huku Barcelona na Paris St-Germain zikimtaka. ***(Goal)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA ATAJWA KUINOA BRAZIL 2026

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anaripotiwa kufanya mazungumzo ya siri juu ya uwezekano wa kuwa kocha mpya wa Brazil mwaka 2026.

**Guardiola anakaribia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na Manchester City na ameapa kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake hivi karibuni, huku ripoti zikisema nyongeza ya mwaka mmoja hadi mwisho wa msimu wa 2025/26 inaweza kusainiwa hivi karibuni.**

Kwa mujibu wa Sport, mpango wa

## ●●● Kocha huyo anakaribia miezi sita ya mwisho kwenye klabu ya Manchester City na...

Brazil kwa Guardiola utaanza 2026 baada ya uchaguzi wa rais wa FA.

Rais wa sasa Ednaldo Rodrigues atamaliza muhula wake Machi 2026 na mshambuliaji wa zamani wa Real Madrid, Ronaldo de Lima anaaminika kuwa yuko tayari kugombea katika uchaguzi huo.

Ronaldo, rais wa sasa wa klabu ya Real Valladolid inayoshiriki LaLiga, inasemekana alitangaza kwa faragha na Guardiola kwa nia ya kuinoa Brazil.

Wawili hao walicheza pamoja wakiwa Barcelona na inaaminika wamekuwa karibu tangu wakati huo, huku kaka yake Guardiola, Pere, ambaye anahusika katika mpango huo wa siri, amefanya kazi na Ronaldo siku za nyuma.

Hadi sasa, Guardiola hajampa Ronaldo jibu sahihi kuhusu mpango huo.

Bosi huyo wa City bado anafikiria kuhusu mustakabali wake katika Uwanja wa Etihad lakini nafasi ya kubadilisha mandhari mwaka wa 2026 inaonekana kuwa wazi.

# KANE: TUCHEL AMERAHISISHIWA KAZI ENGLAND




**LONDON,** England

HARRY Kane amesema kocha mpya anayekuja wa England, Thomas Tuchel atakuwa na wakati mzuri kutokana na kuibuka kwa wachezaji chipukizi ambao wameng'ara baada ya kukosekana kwa wale wenye uzoefu mkubwa wa kimataifa baada ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Jamhuri ya Ireland kwenye uwanja wa Wembley katika Ligi ya Mataifa ya UEFA, juzi.

Kocha huyo wa zamani wa Bayern Munich na Chelsea, Tuchel ataanza rasmi kuinoa England Januari 1, 2025. Ushindi wa Jumapili wa mabao 5-0 dhidi ya Ireland ambao kocha wao, Heimir Hallgrimsson aliutaja kuwa "aibu".

Baada ya kuona wachezaji tisa wakijiondoa kwenye kikosi chake kabla ya mechi hizo mbili na kocha wa muda wa England, Lee Carsley alipanga baadhi ya wachezaji wa chini ya umri wa miaka 21, akiwamo Curtis Jones wa Liverpool, Noni Madueke wa Chelsea na Taylor Harwood-Bellis wa Southampton, ambao alitwaa nao ubingwa wa Euro 2023 kwa vijana chini ya umri wa miaka 21.

Nahodha wa England Kane alisema Tuchel atavuna manufaa ya Carsley kutoka kwa vijana atakapochukua jukumu la kuinoa timu hiyo kufuzu Kombe la Dunia 2026.

"Thomas Tuchel ana wachezaji wengi wa kuchagua," alisema Kane akiiambia ITV.

"Wachezaji wengi wachanga ambao wameingia na kufanya vizuri na baadhi ya wachezaji wenye uzoefu ambao ni majeruhi na watatafuta kurejea ili kuwe na uwiano mzuri. Nina hakika Tuchel atakuwa akimtazama kila mtu. Tulizungumza kuhusu nafasi mpya kwa vijana wapya na wameonyesha ni kwa nini wako hapa."

Kane alianza kuifungia England kwa mkwaju wa penalti dakika ya 53 bao lake la 69 la kimataifa baada ya mlinzi wa Ireland, Liam Scales kutolewa nje kwa kadi nyekundu baada ya kupokea kadi ya pili ya njano kwa kumchezea vibaya Jude Bellingham.

# Neymar akataliwa kwao Brazil

**SAO PAULO,** Brazil

RAIS wa klabu ya Palmeiras ya Brazil amefutilia mbali uwezekano wa kumsajili Neymar akisisitiza kuwa hawana uwezo wa kumsajili mchezaji ambaye ni majeruhi wa kudumu.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona alikuwa mmoja wa majina yaliyotawala vichwa vya habari waliohamia Ligi Kuu ya Saudi Arabia baada ya kuondoka Paris Saint-German, lakini alipata jeraha la goti akiwa kwenye majukumu ya kimataifa hali iliyomfanya kuwa nje ya uwanja kwa kipindi cha zaidi cha mwaka mmoja.

Neymar alirejea tena kwa kucheza mechi mbili za Ligi ya Mabingwa ya Asia, lakini akapata pigo kwa kuumia tena.

Mfungaji huyo bora wa muda wote wa Brazil kwa upande wa wanaume ameichezea Al Hilal mara saba pekee, ambayo inamlipa mishahara mkubwa zaidi, na amekuwa akihusishwa kuondoka Mashariki ya Kati na kurejea nchini kwake.

Timu moja ambayo haitashiriki kumnasa Neymar ni Palmeiras.

Rais wa Palmeiras klabu yenye makazi yake Sao Paulo, Leila Pereira, alisema atarejea katika timu ya zamani ya Santos, lakini wao hawana mpango nae.

Aliiambia UOL: "Mchezaji mzuri, lakini anaenda Santos.

"Neymar hatajiunga na Palmeiras, klabu hii si idara ya matibabu. Nataka mtu ambaye atakuja kujiunga mara moja, ambaye anaweza kucheza kesho kama kocha akitaka.

"Sitakubali tusajili mchezaji ambaye hastahili kucheza."

Neymar alitumia misimu sita akiwa na PSG kabla ya kuondoka Ufaransa, akiwa ameshinda mataji matano ya Ligue 1.






# *Modric atakiwa Dinamo Zagreb*

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Dinamo Zagreb, Nenad Bjelica amemtaka Luka Modric kufikiria kurejea kwa hisia katika kikosi chake cha zamani anapokaribia mwisho wa mkataba wake na Real Madrid.

Modric, aliyefikisha umri wa miaka 39 Septemba, anakaribia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake wa sasa na anakabiliwa na mustakabali usio na uhakika, baada ya kushindwa kuwa na nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha kocha Carlo Ancelotti katika kipindi cha miezi 18 iliyopita.

Kiungo huyo ameanza mechi tano tu kati ya 12 za LaLiga msimu huu, akiwa amefanikiwa kuanza mara 18 msimu uliopita, na anakaribia njia panda katika maisha yake ya soka huku akifikiria kuendelea na Madrid, kustaafu au kuhamia kwingine.

Na sasa bosi wa Dinamo, Bjelica anaona chaguo bora zaidi kwa Modric ni kurejea katika kikosi hicho ambako alijitambulisha kabla ya kujiunga na Tottenham Hotspur mwaka 2008.

"Nani hangependa kuwa na Luka Modric katika timu yake?" aliiambia Radio MARCA.

"Nadhani kila shabiki wa Dinamo Zagreb angefurahi sana kuwa na Luka, angalau kwa mwaka mmoja.

"Hakika angeisaidia timu sana, lakini jambo la kweli zaidi ni kwamba atabaki Madrid au amalizie kibarua chake mahali pengine, ingawa tungependa amalizie soka yake Dinamo Zagreb."

## Yanga yatetea uamuzi kumtimua Gamondi, Ramovic aanza kazi rasmi

INATOKA UK. 24

Kamwe aliwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuiunga mkono timu na kuachana na lawama, kwani viongozi wamefanya uamuzi sahihi na wakati sahihi kuachana na Gamondi na majibu yake yatapatikana uwanjani hivi karibuni.

"Ulikuwa wakati sahihi na tumefanya uamuzi sahihi kuachana na Gamondi, mwisho wa siku uamuzi wa viongozi kwenye mpira majibu yake huwa yanapatikana ndani ya uwanja, hasa yakiwahusisha wachezaji au benchi la ufundi, nadhani muda kidogo umma utaelewa ni kwa nini viongozi walifanya uamuzi huo," alisema Kamwe.

Hata hivyo, alisema hawatoweka sababu yoyote ya kwa nini wamefanya uamuzi hayo, kwani hiyo inabaki kuwa siri ya uongozi na kocha aliyeondoka.

"Hakuna mahala popote duniani ambapo klabu inamwondoa kocha na inaweka hadharani sababu, yale hubaki kwenye meza ya mazungumzo kwa maana hiyo hatuwezi kuweka hadharani kwa nini tumemwondoa, itoshe kusema tu kuwa ukurasa wetu na Gamondi umefungwa," alisema.

Yanga itaumana na Al Hilal Novemba 26, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ukiwa mchezo wa kwanza hatua ya makundi.

## Taifa Stars kufa kupona leo

INATOKA UK. 24

Kongo Jumamosi iliyopita.

Matokeo hayo yamefanya vita ya kufuzu kubaki kwa Stars na Guinea kusaka ushindi ili kuuungana na Kongo kwenda Morocoo kwenye fainali hizo baada ya Ethiopia kutokuwa na matumaini yoyote ya kufuzu kutokana na kuburuza mkia ikiwa na pointi moja pekee.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania, Clifford Ndimbo, alitangaza Rais Samia Suluhu Hassan ametoa ofa kwa mashabiki kuingia bure kuishuhudia timu yao na hakutakuwa na kiingilio.

"Mchezo utaanza saa 10 jioni Uwanja wa Benjamin Mkapa, Rais Samia kuelekea mchezo wa kesho ameagiza mashabiki kuingia bure na mbali na hilo, mashabiki 20,000 wa kwanza watapata zawadi maalum, hakutakuwa na kiingilio kwa mashabiki wote," alisema Ndimbo.

# SIMBA VINARA MABAO YA VICHWA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwangwo**

TIMU ya Simba inaongoza kwa kufunga mabao kwa vichwa kwenye mechi za Ligi Kuu hadi kufikia raundi ya 10 na baadhi ya michezo ya raundi ya 11.

Wachezaji Ibrahim Hamad 'Bacca' wa Yanga, John Makwata wa Coastal Union, Elvis Rupia wa Singida Black Stars na Peter Lwasa wa Kagera Sugar, wanaongoza kwa kufunga mabao mengi kwa njia hiyo.

Simba imepachika mabao manne kwa vichwa katika mabao 25 yaliyopatikana kwa njia hiyo mpaka sasa ambapo Ligi Kuu imesimama kupisha michezo ya kimataifa ya kalenda ya FIFA.

**Kwa mujibu wa takwimu za dawati la michezo Nipashe, jumla ya mabao 164 yamefungwa mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, 94 yakipachikwa kwa mguu wa kulia, 45 kwa mguu wa kushoto na 25 kwa vichwa.**

Simba imefunga mabao yao kupitia wachezaji Che Malone Fondoh, Valentino Mashaka, Edwin Balua na Steven Mukwala.

Timu zinazofuatiwa kwa kufunga mabao mengi kwa vichwa ni Coastal Union, Singida Black Stars, Fountain Gate na Kagera Sugar kila moja ikifunga matatu.

Mabao mawili ya Coastal yalifungwa na Makwata, moja likifungwa na Semfuko Charles, Singida Black Stars mabao yao mawili yamefungwa na Rupia, 1 na Mohamed Damaro, Fountain Gate yakifungwa na Elie Mokono, Nicolaus Gyan na Abalkassim Khamis, huku ya Kagera Sugar 2 yakipachikwa na Lwasa na moja Obrey Chirwa.

Yanga imefunga mabao mawili ya vichwa mpaka sasa, yote yakifungwa na Bacca ambaye ni mmoja wa wachezaji walioongoza kwa kufunga mabao ya vichwa, akiwa pamoja na Makwata wa Coastal, Rupia wa Singida na Lwasa wa Kagera Sugar, wote wakiwa na mabao mawili.

SOKA...



Vijana wanaolelewa katika Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Prisons kuikabili JKT kwenye dabi ya majeshi*

**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa Prisons, Jumanne El Fadhili, amekiri kuwa mchezo wao dhidi ya JKT Tanzania Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam, utakuwa mgumu kwani haijawahi kuwa mechi rahisi zinapocheza timu za majeshi hasa timu hizo mbili.

Akizungumza juzi kuelekea kwenye mchezo huo, El Fadhili alisema katika mchezo huo timu yoyote itakayojipanga vizuri inaweza kuibuka na ushindi huku akiongeza kuwa wao Prisons wapo kwenye maandalizi kabambe kwa ajili ya kuhakikisha wanaibuka na ushindi.

"Hizi ni timu za majeshi na zinajuana, mechi huwa ni ngumu sana, inakuwa na matumizi ya akili na nguvu kwa wakati mmoja, hakuna mchezo wowote rahisi kati yetu na wao (JKT), lakini atakayejipanga vizuri atashinda.

Sisi tutakuwa ugenini wao nyumbani, tunakwenda kwa tahadhari sana, pamoja na hayo hilo halizuii sisi kupambana na kupata matokeo ya ushindi kama tutajipanga vizuri," alisema nahodha huyo.

Naye golikipa wa timu hiyo, Edward Mwakyusa ambaye kwa sasa ameanza kuaminiwa na kuwekwa langoni badala ya Mussa Mbisa, amesema amejipanga kuhakikisha wanapata ushindi katika dabi hiyo ya timu za majeshi.

"Nashukuru kocha ameanza kuniweka langoni, ameanza kuniamini na alikuwa ananiambia we tulia ipo siku utacheza, na kweli, nimeanza kucheza na bahati nzuri nimefanya vizuri sijawaangusha wenzangu na naahidi sitawaangusha katika michezo yote ambayo nitakaa langoni," alisema.

Kipa huyo ameanza kupewa nafasi ya kuanza badala ya kipa namba moja, Mbisa ambaye Kocha Mkuu, Mbwana Makata alikaririwa akisema amekuwa akifanya makosa mengi na kusababisha timu kufungwa mabao mepesi.


Kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Prisons inashika nafasi ya 12 ikiwa na pointi 10 baada ya kucheza mechi 10, ikishinda miwili, sare nne na kupoteza michezo minne.

Prisons itaumana na JKT Tanzania ambayo pia ina pointi 10 baada ya kucheza michezo tisa, ikirejea dimbani kwa mara ya kwanza tangu mwezi uliopita wakati mechi zake zilipoahirishwa kutokana na basi lao kupata ajali jijini Dar es Salaam lilipokuwa likitoka jijini Dodoma kucheza dhidi ya Dodoma Jiji.

Michezo

Jumanne Novemba 19, 2024

Nipashe



Guardiola atajwa kuinoa Brazil 2026 UKURASA 21



Wachezaji wa Taifa Stars wakiongozwa na Nahodha Mbwana Samatta wakishangilia bao kwenye mchezo uliopita dhidi ya Ethiopia wa kufuzu Fainali za Afrika. Stars leo inacheza na Guinea mchezo wa mwisho kwenye kundi lao. **PICHA: TFF**

## Yanga yatetea uamuzi kumtimua Gamondi, Ramovic aanza kazi

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema ulikuwa sahihi kufanya uamuzi wa kumtimua Kocha Miguel Gamondi na kumtangaza Sead Ramovic ambaye jana ameanza rasmi kazi ya kukinoa kikosi cha timu hiyo kuelekea kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema kocha huyo ameshakutana na uongozi na benchi lake la ufundi na watu wa idara mbalimbali, lakini alikuwa hajakutana na wachezaji, ambapo jana alitarajiwa kukutana nao kwenye mazoezi ya timu hiyo na moja kwa moja kuanza kazi rasmi.



"Leo (jana), kocha anatarajia kuanza rasmi kazi ya kukinoa kikosi kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Al Hilal na malengo yetu kwake ni yale yale, kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na kufika robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika, baada ya hapo tutaangalia mengine mbele, kocha yoyote angekuja angeyakuta haya malengo yetu," alisema Kamwe.

Ramovic amechukua mikoba ya Miguel Gamondi ambaye alifutwa kazi wiki iliyopita kwa sababu ambazo uongozi haujaziweka wazi, ingawa ni baada ya kupata vipigo viwili mfululizo kwenye Ligi Kuu.

INAENDELEA UKURASA 23

# Taifa Stars kufa kupona leo

**Na Faustine Feliciane**

### ●●● Kocha Moroco asema haijawahi kufuzu Afcon kirahisi rahisi, Rais Samia aagiza mashabiki kuingia bure huku...

KOCHA wa Timu ya Soka ya Taifa 'Taifa Stars', Hemed Suleiman ' Moroco', amesema timu hiyo haijawahi kufuzu Fainali za Afrika (AFCON) kirahisi rahisi hivyo leo itakuwa na kazi moja tu ya kupambana kuhakikisha wanapata ushindi mbele ya Guinea na kufuzu kwa mara ya nne fainali hizo za mwakani zitakazofanyika nchini Morocco.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam kuelekea kwenye mchezo huo, Moroco alisema mechi ya leo itakuwa ya mwisho kwenye kundi lao inayohitaji maamuzi na wapo tayari kupambana kadri ya uwezo wao kuhakikisha Stars inapata ushindi.

Kwenye mchezo wa leo Stars inahitaji ushindi tu kuweza kufuzu fainali hizo kwani itakuwa imefikisha pointi 10 na kushika nafasi ya pili kwenye kundi lao linaloongozwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo wenye pointi 12.

**Kufungwa au sare yoyote kutatoa nafasi kwa Guinea kuungana na Kongo kwenda Morocco kushiriki fainali hizo za Morocco.**

Endapo Guinea itashinda mchezo wa leo itafikisha pointi 12 na ikitoa sare itafikisha pointi 10 na kufuzu fainali hizo kuiacha katika nafasi ya tatu Taifa Stars.

"Tuko vizuri wakati huu kuliko wakati wowote, wachezaji na benchi la ufundi wanajua umuhimu wa mchezo wa kesho (leo), bado sijawa na presha yoyote na naamini tutapata matokeo mazuri, hatujawahi kuingia AFCON kirahisi rahisi, hivyo kwa uzoefu wangu mechi ya mwisho ndio inafanya maamuzi," alisema Moroco.

Alisema Watanzania watokeze kwa wingi na kuiombea timu hiyo kuweza kupata matokeo mazuri yatakayowapeleka kwenye fainali za AFCON.

Nahodha wa Stars, Mbwana Samatta, amesema kama wachezaji wanafahamu umuhimu wa mchezo wa leo na wapo tayari kupambana mpaka filimbi ya mwisho kuhakikisha wanapata ushindi na kufuzu AFCON.

"Ni mechi muhimu sana kwetu, kila mchezaji anafahamu umuhimu wake, tupo tayari kupambana kwa ajili ya taifa letu kuhakikisha tunafuzu tena AFCON, tutapambana kupata ushindi," alisema Samatta.

Nafasi ya kufuzu kuungana na Kongo imebaki kwa Stars na Guine ambazo zinashika nafasi ya tatu na ya pili baada ya Stars kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ethiopia na Guine kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >